APRILI MMXXV - TOLEO LA XLII

# NGURUMO
*ya Mwandishi*



**RIWAYA:**

MSALITI '03' uk 12-13
HAPPY NEW YEAR '4' uk 26-27
SHEMEJI USIZIME TAA '5' uk 28-29

# JENEZA LA TAIFA

## YALIYOMO

**TAHARIRI**— MAZIWA YA KUKU… — Uk 02

**MWANDISHI WETU**— Godlove Kabati — Uk 03

**New In Town:** Mwandae Mtoto wa Kiume Kuwa Mwanaume **—** 04

**PITIO LA VITABU**— KILIO CHETU '1'—Uk 06

**MAKALA** — **SAIKOLOJIA**: Saikolojia na Mapenzi—Uk 07

**MAKALA:** Umuhimu wa Fasihi kwa Mwanadamu…-uk 08

**MIAMBA WA AFRIKA:** PATRICE LUMUMBA '5'— Uk 10

**SAKO KWA BAKO –** Rose Camillus Nyandindi **—**Uk 11

**RIWAYA:**— MSALITI '3'—Uk 12 na 13

**RIWAYA—** Najutia Kuwa Na Wewe '2'**-** Uk 14 na 15

**YA KALE NI DHAHABU**: — Alibaba na Wezi 40 '18'- Uk 16

**HABARI:** TUZO YA TAIFA YA MWL. NYERERE – Uk 17

**SHUBAKA LA VITABU:** HISTORIA YA VITABU 'Kitabu cha Wafu'—Uk 18

**KITABU NILICHOSOMA:** UJANAJIKE —Uk 19

**MATANGAZO: -** Uk 20

**MALENGA WA KILEO:** Nawapongeza washindi — Uk 21

**HABARI PICHA: -** TUZO ZA TUCHAWA-Uk 22

**KUTOKA MAKTABA:** Maisha ni Mapambano '8'-Uk 23

**ELIMU JAMII:** — Mabadiliko ya Tabia Nchi —Uk 24

**HADITHI:** — Happy New Year '4' Uk. 26 na SHEMEJI USIZIME TAA…!

## TAHARIRI:
# JENEZA LA TAIFA

Salaam kwenu nyote,

JENEZA LA TAIFA ndiyo wimbo wa mjini. Natumai nyote mu wazima kabisa bukheri wa afya. Mimi mtumishi wenu nisiye na faida nakusalimuni kwa jina la Fasihi ya Kiswahili… usomaji uendelee!

Mwezi wa Aprili tumeshuhudia Tuzo ya Taifa ya Mwalimu Nyerere ya Uandishi Bunifu ikilitikisa jiji na nchi nzima kwa ujumla. Hii ni tuzo iliyo chini ya serikali na inasimamiwa na Wizara ya Elimu kupitia Taasisi ya Elimu Tanzania. Msimu wa tatu sasa umemalizika na hivi punde tu yataanza makusanyo ya msimu wa nne.

Nilipojaribu kufuatilia kwa undani nimegundua kuwa mpaka msimu huu wa tatu katika upande wa riwaya, washindi wote wametokea UWARIDI. Sikuamini, ikabidi nirudie tena na tena. Ni kweli; msimu wa kwanza alinyakua Hamisi Kibari, Msimu wa pili Laura Pettie na sasa ni maundu Mwingizi. Hii inabeba taswira halisi ya UWARIDI kuwa ni waandishi wa riwaya wenye dira. Aisee kongole kwao sana.

Jeneza la Taifa, ndiyo riwaya iliyompa ushindi Bwana Maundu Mwingizi aambaye kila mpenda fasihi anajua jinsi gani kijana huyu anajua kucheza na kalamu katika kukipambaa Kiswahili, mpaka wapenzi wa mwandiko wake wakampa rakabu 'Mwanabalagha'.

Sisi Ngurumo ya Mwandishi tunawaahidi tutamtafuta huyu bwana tuzungumze naye juu ya siri ya yeye kukijua Kiswahili namna ile. Ijapokuwa ni mtu wa kujificha sana lakini tutajitahidi tumpate ili atujibu maswali yetu kwa niaba yenu.

Basi wapenzi wasomaji, endeleeni kuburudika na jarida lenu pendwa la kifasihi. Na msisite kutupa mrejesho wa burudani mnazopata humu.

Amani iwe kwenu!
Richard Richard Mwambe
Mbeya, Mei 2025

**NGURUMO YA MWANDISHI**

**WASILIANA NASI**
**0766 974 865 AU 0627160016**
**WhatsApp: +255 766974865**

## MWANDISHI WETU:
## GODLOVE KABATI

**KARIBU tena mpenzi msomaji wa jarida letu. Lakini kwa namna ya pekee wewe mdau wa fasihi unayependa kujua kuhusu fasihi na wanafasihi. Leo katika safu yetu ya Mwandishi Wetu, tupo na kijana machachari katika uandishi wa riwaya ambaye anachipuki kwa nguvu. Ni nani huyu?**

**Ungana nasi ili kumjua vyema na kisha m- 'follow'**



GODLOVE KABATI

Naam!

Kwa majina naitwa GODLOVE KABATI.

Ni mwenyeji wa Bukoba Kagera japo kwa sasa naishi mkoani Morogoro kimasomo. Mimi ni mwanachuo, ninasoma shahada ya udaktari wa wanyama katika chuo kikuu cha kilimo SOKOINE.

Godlove ni mwandishi anayechipukia kwenye ulingo huu wa sanaa ya fasihi. Ni mtunzi na mwandishi wa makala mbalimbali, mashairi, simulizi na riwaya.

Nakiri kuwa nimetokea kwenye familia iliyokumbatia sana utamaduni wa kusoma riwaya na simulizi. Nakumbuka nilikuwa nikimuomba sana dada yangu anisomee japo kurasa chache tu za simulizi mbalimbali.

Hata nilipoanza shule sikuruhusu riwaya au kitabu chochote kile cha hadithi ya Kiswahili kikatize bila kukaguliwa na macho yangu.

Kama utani, nikavutiwa na kile kilichofanywa na sanaa ya uandishi wa Marehemu Ben R. Mtobwa, hayati Shaaban Robert, Bwana Hussein Issa Tuwa na wengine wengi niliosoma riwaya zao kipindi kile. Bila kusukumwa wala kusurutishwa na mtu, nami nikajikuta napenda kutunga na kuandika hadithi.

Sijafanikiwa kutoa kitabu chochote mpaka sasa, hii ni ndoto yangu kubwa ya muda mrefu. Tayari nimeandika na bado ninaandika miswada mbalimbali ambayo hakika siku moja kwa msaada wa Mwenyezi, itakuwa vitabuni.

Changamoto ninazokutana nazo katika uandishi ni nyingi. Haswaa kwa upande wangu mimi kama mwandishi chipukizi;

Kwanza kabisa, kama tujuavyo uandishi wa fasihi ni sanaa inayotegemea uhai wa fanani na hadhira yake ili iishi. Changamoto kubwa ni huo uhai wa hadhira...

Waweza kuandika kazi yako na wasomaji wako wakaipenda lakini wakabaki kimya kabisa! Bila kutoa maoni yoyote yale, hali hii hukatisha tamaa.

Pia changamoto nyingine ambayo nimejifunza kukubaliana nayo ni kuwa uandishi ni kazi inayohitaji uwekezaji mkubwa wa muda, nguvu na utafiti wa kipekee. Ukizingatia kuwa mie bado ni mwanafunzi na masomo yangu ya tiba yananidai uzito uleule...nimejikuta nikihairisha baadhi ya nyakati zangu chache za kustarehe nikiitumikia fasihi!

Pia wapo wasomaji wadokozi (kama kweli wanastahili kuitwa wasomaji), hili ni kundi la viumbe wanaoiba kazi ya mwandishi kisha wanabadilisha jina na kujinadi kuwa wametunga wao.

Kwa maoni yangu, soko la vitabu linategemea hasa na ubora wa maandishi ya mtunzi husika. Hivyo, ni utunzi wenye ubora wa hali ya juu utakaoinua soko la vitabu. Vilevile ushirikiano miongoni mwa waandishi hasa kupitia vyama mbalimbali, hili litachochea moto ununuzi wa vitabu vyetu.

Waandishi wanaonivutia hapa nchini ni wengi ila ninaowahusudu zaidi ni legend George Iron Mosenya, Abyas Mzigua na Nyemo Chilongani. Pia navutiwa sana na uandishi wa makala za Kaisal Ally, Azizi Kasese pamoja na kaka Twahir Yusuph.Kwa sasa kazi zangu zinapatikana kwenye ukurasa wangu wa Facebook kwa jina la KALAMU YA KABATI pamoja na MAJIVU YA FASIHI WhatsApp channel. Pia katika majukwaa ya burudani kuleee, Jamii Forums! **Godlove Kabati 0763204351.**

## NEW IN TOWN :

KUHUSU KITABU
MALEZI ni wajibu usio na kikomo ambao binadamu humsaidia mwingine kujitambua na kukua kiakili katika maisha.

Kitabu cha Mwandae Mtoto wa Kiume kuwa Mwanaume kimejikita katika falsafa ya malezi ambayo inawezesha kumjenga mtoto wa kiume.

Katika falsafa ya malezi ni muhimu Mzazi au Mlezi kuchagua njia bora za kumtengeneza mtoto wa kiume kuwa mwanaume bora. Kitabu pia kinaangazia namna ya kumlinda katika usalama, kumwezesha kiuchumi, kumshauri, kumwelimisha na kumkuza kihisia na kimwili.


Kumwezesha kuyaelewa mazingira yake, uhusiano na watu, mabadiliko ya mwili wake, matamanio yake, ndoto zake, njia zake, kipaji chake, shujaa wake na namna bora ambayo mzazi au Mlezi angependa kuona mtoto wake wa kiume anakuwa sehemu ya jamii bora.

Kama tujuavyo, malezi si kazi ya watu wavivu wala si lelemama bali inahitaji kuvumilia, kuelekeza, kupenda na kuzingatia njia sahihi za kumkuza.

Katika falsafa ya malezi ni kama mfano wa Bata na Kuku.
• Bata anapokuwa kwenye matembezi hutangulia mbele huku vifaranga vyake humfuata nyuma.
•Kuku hutanguliza mbele vifaranga vyake kwenye matembezi yao huku akivituata nyuma.

Je wewe mzazi una malezi ya aina gani Kwa mtoto wa kiume? Ni malezi ya Bata au kuku?

Vilevile kitabu kinaweka misingi kwa wazazi na Walezi katika jukumu lao la kuwafundisha watoto wa kiume mbinu mbalimbali za maisha zenye mguso wa kipekee.
Hayo na mengine mengi utayasoma kitabuni humu.
HANIFA KAFASHE






# KILIO CHETU—1

## PITIO LA VITABU




www.richardmwambe.com
JAMVI la SIMULIZI

TAMTHILIYA; KILIO CHETU

MWANDISHI; MEDICAL AID FOUNDATION

MCHAPISHAJI; TANZANIA PUBLISHING HOUSE

MWAKA; 1995

JINA LA MHAKIKI; Mwalimu Daud Makoba

Kilio chetu ni tamthiliya inayovunja ukimya uliotawala miongoni mwa jamii katika kutatua matatizo makubwa ambayo chimbuko lake ni mahusiano ya kijinsia.

Katika tamthiliya hii vijana wanatoa sauti ya jitimai iliyojaa sononeko na shutuma dhidi ya wazazi, walezi na viongozi ambao wanafumbia macho suala hili nyeti. Ndiyo maana tamthiliya hii inasisitiza sana haja ya kuwapa vijana elimu juu ya mahusiano ya kijinsia badala ya hofu na vitisho ambavyo vimedhihirika kupitia hali halisi ya kuwa vimeshindwa.

FANI

MUUNDO

Tamthiliya hii imetumia muundo wa moja kwa moja. Inaanza kwa kutuonesha wazazi wakibishana juu ya kutoa elimu ya jinsia na mahusiano. Mwisho Joti mtoto ambaye hakupatiwa elimu hiyo anampa mimba mtoto mwenzake Suzi. Baadae Joti anakufa kwa UKIMWI.

Pia tamthiliya hii imegawanywa katika sehemu sita.

sehemu ya kwanza. Inaonesha jinsi ambavyo gonjwa la UKIMWI linaiteketeza, jamii wengi wao wakiwa watoto ambao hawakuwa na elimu ya jinsia na mahusiano.

sehemu ya pili. Wazazi wanabishana juu ya kuwapatia elimu ya jinsia na mahusiano watoto wao. Mama Suzi anasema jambo hilo liko kinyume na maadili, lakini Baba Anna yeye anaunga mkono suala hilo.

sehemu ya tatu. Inaeleza kuhusu watoto Joti na Suzi ambao wamekwisha anza mambo ya ngono. Pia watoto wameathiriwa na utandawazi kwani wanaangalia video za ngono bila wasiwasi.

Sehemu ya nne. Inazungumzia tabia hatarishi za Joti kuwa na wasichana wengi. Vilevile Anna kutokana na elimu ya jinsia na mahusiano aliyonayo, anaendelea kukwepa vishawishi.

Sehemu ya tano. Mtoto Suzi kapata mimba, anabaki njia panda akiwa hajui afanye nini.

MTINDO

Tamthiliya hii imetumia mtindo wa;

i. Dayolojia – majibizano ya wahusika yametawala toka mwanzo mpaka mwisho wa tamthiliya hii.

ii. Monolojia – mtindo huu wa masimulizi umetumika japo kwa kiasi kidogo.

iii. Mtindo wa masimulizi ya ki ngano - mfano katika ukurasa wa 1 Mtambaji anasimulia,

> "Hapo zamani za kale paliondokea kisiwa kimoja kikubwa sana. Kisiwa kilikuwa na watu wa kila aina…"

iv. Matumizi ya nyimbo – katika ukurasa wa 29, Anna anaimba wimbo unaokemea wanaume wanaomfuata kumlaghai.

> "Anna, Anna, Anna mie niacheni mie x 2
>
> Msichana mdogo bado ninasoma niacheni mie."

v. Matumizi ya nafsi

Nafsi zote zimetumika lakini nafsi ya pili imetawala zaidi.

SOMA VITABU

- Kwa afya ya ubongo wako
- Kwa kujiongezea maarifa
- Kwa burudani

USISITE

- Kumsimulia mwingine hadithi uliyosoma
- Kumfundisha mwingine yale uliyojifunza
- Kumshauri mwingine kitabu cha kusoma

NI VIZURI

- Kutembelea maktaba
- Maduka ya vitabu
- Kupiga stori na waandishi

# SAIKOLOJIA NA MAPENZI



## UHUSIANO KATI YA UTIMAMU WA AKILI NA UFANYWAJI WA MAPENZI.

Habari ya wakati huu mpendwa wangu, sina shaka u buheri wa afya tele na u timamu kiakili. Na kama ni hivyo, basi mshukuru Mungu, na ikiwa una changamoto yoyote iwe kiafya au ki mwili ama katika maisha kwa kupitia mitihani mbali mbali ya maisha,usichoke kumuomba Mungu na kumshukuru Yeye katika yote. Jikite pia kwenye kusuluhisha matatizo yanayokusonga.

Katika toleo hili tuone uhusiano uliopo kati ya utimamu wa afya ya akili na ufanywaji wa mapenzi.

Unapozungumzia afya ya akili unazungumzia hali ya kuwa sawa kichwani/kifikra. Ni rahisi sana kugundua kama akili yako haipo sawa kwani mmiliki wa akili ni wewe mwenyewe hivyo utakavyohisi kukosa utimamu wa akili unapaswa kujiuliza ni nini chanzo cha kutokua sawa.

Yapo mambo mengi ambayo yanaweza kupelekea akili ya mtu kutokua sawa. Leo tuangazie uhusiano uliopo kati ya ufanywaji mapenzi na utimilivu wa akili yako.

Afya ya akili inahusianishwa moja kwa moja na ufanywaji wa mapenzi wakati mwingine. Kuna wakati mtu mzima huwa na mhemko wa hasira kiasi cha kuwa anakua mkali mkali muda wote, sababu zinaweza kuwa nyingi nyingi kulingana na mazingira husika ya wakati huo lakini pia wakati mwingine kama hajashiriki tendo la kujamiiana muda mrefu nayo inaweza kuwa sababu.

Kufanya mapenzi kwa mtu timamu aliyetimia kiakili na kimwili, anakula vyakula na kushiba kila wakati, ni muhimu kufanya mapenzi ili kuuridhisha moyo, mwili na akili pia.

## MADHARA YA KUTOFANYA MAPENZI.

### 1. UPWEKE.

Ikiwa mwanamke au mwanaume asipofanya mapenzi/asipojamiiana kwa muda mrefu itamletea hali ya upweke kupitiliza. Muda mwingi atajikuta anatamani kuwa peke yake, wakati mwingine anaweza kujitenga na watu na kumfanya awe mtu wa kukaa peke yake muda mwingi. Hali ya upweke inaweza kumkumba mtu asiyejihusisha na mahusiano/kushindwa kufanya mapenzi. Upweke ni ugonjwa wa kisaikolojia, na hivyo usipojihusisha na mahusiano muda mrefu ni moja kwa moja utapatwa na maradhi ya kisaikolojia kama UPWEKE.

### 2. UKIMYA/UPOLE KUPITILIZA.

Usipokua kwenye mahusiano,/ usipofanya mapenzi muda mrefu, unaweza kupatwa na hali ya kuzubaa/ukimya uliopitiliza/upole uliopitiliza, waswahili wanaita unakua zebwe/bwege yaani unakua ni mtu uliepooza sana. Wapo watu wasipofanya mapenzi kwa muda mrefu, hukumbwa na hali ya kuwa mpole kupitiliza au ya kuwa mkimya kupita kiasi, akikaa mahali ni mpaka anaonyesha kuzubaa kabisa. Hali hiyo inahusishwa na madhara ya kisaikolojia moja kwa moja.

# SAIKOLOJIA NA MAPENZI

**3. UKALI/UKOROFI KUPITILIZA.**

Wapo baadhi ya watu huwa wakali sana, yaani kwa kila jambo anakua mkali mkali tuu, licha ya kuwa anaweza kuwa aliumbwa kuwa mkali mkali lakini pia anaweza kupata hali ya ukali kutokana na kushindikana kutolewa kwa vichochezi vya *hormone* iitwayo "kisspeptin", KISSPEPTIN ni hormone inayochochea hamu ya ufanisi wa tendo la ndoa, hormone hii huwa inazalishwa katika mwili wa binadamu kutoka kwenye ubongo ili kuchochea hamu ya kufanya mapenzi.

Hormone hii inapozalishwa hutakiwa kufanya kazi au kutolewa muda wa kufanya mapenzi kupitia utolewaji wa "shahawa" au manii kwa pande zote mbili yaani jinsia ya me na ke. Hormone hii inapozalishwa halafu ikashindwa kufanya kazi husika hugeuka kuwa sumu dutu katika akili ya mwanadamu hivyo inaweza kupelekea mtu husika kuwa mkali au mkorofi kupitiliza.

Ni vyema pia kuzingatia ufanywaji salama wa mapenzi, sio kwa kuwa usipofanya mapenzi unapata madhara ya kisaikolojia basi ndio uwe mfanyaji wa msapenzi kiholela lah - hasha, zingatia usalama wa afya yako ya kimwili na kiroho hasa ukizingatia pia ufanyaji mapenzi na watu tofauti tofauti unaweza kukuletea madhara kiroho kwa kuruhusu roho chafu kukuandama.

Mliopo ndoani, saidieni jamii katika swala hili, kama upo katika ndoa inayotambulika kiserikali mpaka kimira au kidini, zingatieni kuhudumiana kimwili pale mnapohitajiana. Ufanywaji mapenzi uwe kwa kiwango kizuri kiasi cha wote kuridhishana. Peaneni vijizawadi vidogo vidogo ili kunogesha penzi lenu. Hurumianeni, pendaneni kweli na pia msinyimane tendo ili kuepuka kupeana madhara kisaikolojia.

Karibu upate vitabu:

SAIKOLOJIA YA MAHUSIANO NA NDOA… Tsh.12,000, na JITIBIE KISAIKOLOJIA… Tsh.10,000. Tembelea ukurasa wangu wa Facebook wenye jina Neema Mgao ili kupata taarifa Zaidi au wasiliana na mimi kupitia +255 763 013 206 ili kujua namna ya kupata vitabu hivyo. Karibu sana.

ASANTE.

**The Magic Author,**

**Queen of psychology,**

**MADAME NEEME MGAO.**

*Inatoka ukurasa wa 29*

SHEMEJI USIZIME TAA… NAOGOPA UKIMWI

...nikajua ni pombe zilikuwa zikimsumbua, aibu haikuwepo.

"Ukitaka niwashe taa, kaa kwa adabu na unielekeze aliko Ray upesi" nilifoka.

"Aaah shemeji, hutaniwi" alisema na kuangua kicheko, akanipiga kofi laini na kunirushia busu la mbali. Sikusema neno.

"Shemeji, Ray alipiga simu akasema nikwambia angekuja, lakini ameshindwa kuja,"

"Shemeji utani sipendi, wacha nikurudishe nyumbani, naona umeamua kunisumbua" nilisema kinyonge nikionesha kukerwa. Hilda alinitazama, akacheka, na kurudia kukaa tena kihasara hasara.

"Siyo kukusumbua, Ray naye amezidi kukusifia mpaka naona donge, na kutamani kujua udereva wako" alitoboa ukweli ambao ulizidi kunidhihirishia Ray alikolea sana kwangu.

"Hizo pombe zitakupeleka kubaya, utamtamanije shemejiyo, halafu usipende kujirahisisha hivyo, ukimwi upo na unaua" nilisema na kuzima taa, nikaendesha gari na kumrudisha Hilda, ambaye aliendelea kunilalia begani wakati naendesha. Nilimfikisha, akashuka, na hapo ndipo aliponitolea kali ya milenia.

"Shemeji, ukimwacha dada Ray mi nitakuwa wako. Sauti yake ya mlegezo ilinitesa, nikamjibu.


"Shemeji Ray simwachi… naogopa ukimwi,"

"He! Kwaheri" alisema na kunifinya, akaondoka na nikajua Hilda ni shemeji wa Darisalama na kama nisingekuwa 'ngangari', Mungu anajua.

**MWISHO**

# TAFAKARI YA MWAFRIKA

## TWAJIFUNZA KWA ANDANENGA



© Mwafrika Merinyo*

Wanadamu tumeumbwa na hisia. Hisia ndiyo kielelezo cha athari zitupatazo tunapokutana, kuingiliana, kusigana au kukabiliana kwa vyovyote na ulimwengu au mazingira tuliyomo. Athari zitokanazo na miingiliano hiyo, na mrejesho wa kisaikolojia wa mhusika, navyo aghalabu vimekuwa kipimo cha uwezo wa mwanadamu kuhilimi miingiliano hiyo katika ima kujihifadhi na kujiokoa na miingiliano hiyo au kutumia miingiliano hiyo kama fursa kujinufaisha nayo kwa ustawi wake.

Aidha katika kipimo hiki cha uhimilivu ndipo tuwezapo kuupima uwezo wa mwanadamu kuukubali ukweli wa uhalisia wa mazingira yake na kuukiri wazi ajapozidiwa kimhemko.

Mei Mosi 2025 ulitimia mwaka mmoja tangia mauko ya mshairi gwiji katika ushairi wa Kiswahili, Amiri Abdallah Sudi Andanenga, aliyeenda kwa lakabu ya Sauti ya Kiza. Ushairi wa Andanenga na kazi alizotunga zimetoa ushahidi thabiti kwamba alikuwa gwiji miongoni mwa magwiji, alikuwa jabari katika majabari na alikaribia kileleni mwa mlima wa malenga wa mashairi ya Kiswahili nchini.

Kwa nini naandika tafakuri hii kuhusu Andanenga? Waama ni kwa sababu ya sanaa yake na namna alivyowagusa hadhira yake; lakini zaidi namna alivyozimudu na kuzidhibiti hisia zake kwa kuzitumia kama sehemu ya mafunzo kwa wanadamu wenzie. Tunatambua kwamba katika kupata hisia za kibinadamu msanii hana tafauti yoyote na mtu asiye msanii. Msanii anajitafautisha tu kwa uwezo wake wa kuelezea hisia zake na mawazo yake kupitia sanaa ilihali akitumia fursa hiyo kuwaasa, kuwafunda na kuwaburudisha sawia hadhira yake. Kama msanii, Andanenga alikuwa na umahiri uliopea katika kuelezea hisia zake kupitia ushairi. Kwa leo nitapenda kutumia shairi moja la gwiji Andanenga kuelezea kiini cha hoja yangu. Shairi hili si jingine bali lile lililobeba anuani ya VIPI MBONA MWANITUPA? Alilitunga baada ya kupatwa ugonjwa wa macho ambao ulimsababisha kupoteza uoni maisha yake yote.

Andanenga, katika utunzi wa shairi la VIPI MBONA MWANITUPA? anatoa hisia zake kwa kishindo na mguso mkuu, akiwasuta malenga wenzake kwa 'kumtupa' katika hali ya ugonjwa mbaya ule uliomnyang'anya macho yake. Imezoeleka kwamba watu wapatwapo na majanga ya kustahili kuhurumiwa, hunyong'onyea katika upweke ilihali wakitamani kupata walau faraja ya kutembelewa na kutakwa hali, hata kama si kupewa dawa ya majanga yaliyowasibu. Watu wamechukua mazoea haya kama ishara ya unyenyekevu na, labda, kutotaka kuonekana wanajipendelea au hata kuwasumbua wengine kama ndugu, rafiki na jamaa zao kwa maradhi yao.

Lakini Andanenga, kama msanii, anavunja uzowefu huu na kufanya mapinduzi. Anadai haki yake ya kupata upendo na faraja katika masahibu yake. Katika ubeti wa kwanza anawaambia malenga wenzake Staharaki, Gumu Ganda, Masudi, Litaka na Moyoladi:

*Ikiwa sinayo haki, kunionya yenu budi*
*Kunizuru hamtaki, ni lipi lenu kusudi?*

*Ndugu zangu Staharaki, Gumu Ganda na Masudi*
*Litaka na Moyoladi, vipi mbona mwanitupa?*

Anawasihi wamweleze kama ana kosa hata wamtenge, na wampe sababu za kutomzuru katika adha iliyomsibu. Katika ubeti wa pili anamshukuru Mtu Chake kwa kumtembelea walau mara moja, japo kwamba nayo haikumridhisha sana moyoni *(haidhuru inadhuru);* lakini anaendelea kwa kuwahimiza Nyoka, Halimoja, Ndumba Yiyi na Kingaru wajitahidi kumtembelea *(Shimeni mje nizuru):*

*Mtu Chake ulikuja, siku moja nashukuru*
*Kuongeza huna haja, haidhuru inadhuru*
*Na Nyoka na Halimoja, Ndumba Yiyi na Kingaru*
*Shimeni mje nizuru, vipi mbona mwanitupa?*


Marehemu Amir A. Sudi Andanenga (Sauti ya Kiza)

Ubeti wa tatu ulibeba uzito wa kipekee, kwani aliutumia ubeti wote kumnasihi malenga na gwiji mwingine wa ushairi wa Kiswahili, Abdilatif Abdalla kwenda kumzuru. Bila shaka Abdilatif Abdalla alishika nafasi ya kipekee katika nafsi ya Andanenga. Anamwambia:
*U wapi Abdilatifu, mtunzi ulokubuu*
*Jihimize jikalifu, inua yako maguu*
*Hali uje unishufu, siku moja mwaka huu*
*Bado sijajinafuu, vipi mbona mwanitupa?*

Abdilatif Abdalla alikuwa swahiba yake Andanenga wakiwa na ukuruba wa kifani na upendo wa kidugu; na katika kufahamiana kwao Abdilatif alishamtembelea Andanenga si chini ya mara nne kwa kumbukumbu za Abdilatif. Mwaka 2020 alimtembelea nyumbani kwake Kinondoni Shamba kisha wakaonana mara ya mwisho mwaka 2023 kwenye hafla ya Tuzo za Mwalimu Nyerere za Uandishi Bunifu kabla ya mauko yake Andanenga.

Mifano niliyotoa yatosha kuonesha nguvu ya utunzi na umahiri wa Andanenga katika kuelezea hisia zake kisanii. Jambo kubwa nililoona katika shairi hili ni ujasiri wa kuelezea ukweli wa hisia zake. Andanenga hadai huruma tu, bali anakumbushia wajibu wa mwanadamu kumjali mwanadamu mwenzake. Hili analidhihirisha kwenye ubeti wa tano anaposema

“*Wajibu unawaonya, kwa sime mnaukata?*”

Anawauliza malenga wenzake kama kweli wameamua kuukata kwa sime wajibu wao:

*Mu wapi Shekhe Kanyunya, Kiwato na Kitokota*
*Matimbwa kweli yang'wenya, Babu Jinga pia Chata*
*Wajibu unawaonya, kwa sime mnaukata?*
*Juma Issa na Matuta, vipi mbona mwanitupa?*

Andanenga hakomi hapo, azidisha kuwakumbusha malenga wenzake kwamba kumzuru na kumfadhili mgonjwa ni amri ya Mungu kuhusu upendo miongoni mwa wanadamu:

*Shekhe Mohamedi Ali, na ndugu yako Kibao*
*Msiwate ufadhili, ni wajibu upasao*
*Pendo sifa ya Jalali, mngendemene ni tao*
*Wa bara na wa mwambao, vipi mbona mwanitupa?*

Yafaa kuzingatiwa kwamba kwa Andanenga kutunga shairi hili, kamwe hakuwa anajitetea, kulalamika wala kutaka huruma ya malenga wenzake wa ushairi. Alitumia ushairi wake kukumbusha wanadamu wenzake kuhusu wajibu katika kupendana, kujaliana, kuhurumiana na kuishi kama ndugu. Kwamba hata tuwamo katika changamoto, adha au mateso ya kidunia tusisahau wajibu wetu pia wa kukumbushana kutendeana mema. Naam, yatukumbusha shairi lake jengine, NYEGE NI KUNYEGEZANA.

Salaam aleykum!
02 Mei 2025 Dar es Salaam

**KATIKA safu yetu ya MIAMBA WA AFRIKA, leo tunakuletea Patrice Lumumba. Huyu alikuwa Waziri Mkuu wa nchi ya Congo DRC. Ni mmoja kati ya waafrika wachache waliokataa kuwa vibaraka wa wakoloni, alipambana kuikomboa Kongo, lakini nini kilimkuta? Tuendelee...**



## KIFO CHA LUMUMBA

Tarehe 3 Desemba 1960, kwanza Lumumba alipelekwa kwenye kambi ya jeshi ya Thysville katika Camp Hardy, kilomita 150 (takriban maili 100) kutoka Léopoldville. Aliandamana na Maurice Mpolo na Joseph Okito, washirika wake wa kisiasa waliokuwa wamepanga kumsaidia kuunda serikali mpya.

Walilishwa vibaya na walinzi wa gereza kwa maagizo ya Mobutu. Katika barua yake ya mwisho iliyorekodiwa, Lumumba aliandika kwa Rajeshwar Dayal, mkuu wa Umoja wa Mataifa nchini Congo: *"Kwa kifupi, tunaishi katika hali zisizowezekana kabisa; zaidi ya hayo, ni kinyume cha sheria."*

Asubuhi ya tarehe 13 Januari 1961, nidhamu katika Camp Hardy ilidhoofika. Wanajeshi waligoma kufanya kazi isipokuwa walipwe; walipokea jumla ya faranga 400,000 ($8,000) kutoka kwa Baraza la Mawaziri la Katanga. Baadhi yao waliunga mkono kuachiliwa kwa Lumumba, huku wengine wakiamini alikuwa hatari. Kasa-Vubu, Mobutu, Waziri wa Mambo ya Nje Justin Marie Bomboko, na Mkuu wa Idara ya Usalama Victor Nendaka Bika walifika binafsi kambini humo na kujadiliana na wanajeshi. Migogoro iliepukwa, lakini ikawa wazi kuwa kumshikilia mfungwa tata kama huyo kambini kulikuwa hatari kubwa. Harold Charles d'Aspremont Lynden, Waziri wa mwisho wa Wakoloni wa Ubelgiji, aliamuru Lumumba, Mpolo, na Okito wapelekwe katika Jimbo la Katanga.

Lumumba alifungwa kwa nguvu katika ndege kuelekea Elisabethville tarehe 17 Januari 1961.

Walipowasili, yeye na wenzake waliwekwa chini ya ulinzi na kupelekwa katika Nyumba ya Brouwez, ambako walipigwa vibaya na kuteswa na maafisa wa Katanga, huku Rais Tshombe na baraza lake la mawaziri wakijadili nini cha kufanya naye.

Usiku huo huo, Lumumba, Mpolo, na Okito walichukuliwa hadi porini ambako vikosi vitatu vya kupiga risasi vilikuwa vimekusanywa chini ya uongozi wa afisa wa mkataba wa Ubelgiji Julien Gat. Amri ya kuwaua Lumumba ilitolewa na viongozi wa Katanga. Hatua ya mwisho ya utekelezaji huo ilifanywa binafsi na maafisa wa mkataba wa Ubelgiji wakiongozwa na Kamishna wa Polisi Frans Verscheure.

Lumumba, Mpolo, na Okito waliwekwa mbele ya mti na kupigwa risasi mmoja baada ya mwingine. Utekaji huu unadhaniwa kufanyika tarehe 17 Januari 1961, kati ya saa 3:40 na 3:43 usiku kwa mujibu wa uchunguzi wa baadaye wa bunge la Ubelgiji. Tshombe, mawaziri wengine wawili, na maafisa wanne wa Ubelgiji waliokuwa chini ya mamlaka ya Katanga walikuwepo. Miili yao ilitupwa katika kaburi la juujuu.

***MWISHO***



# SAKO KWA BAKO:

## Madam Rose: mwalimu wa lugha mwenye haiba yake

SAFU yetu ya Sako Kwa Bako imeendelea kuchanja mbuga. Na katika toleo hili inakutana na huyu Mwalimu, mchangamfu, mwongeaji mzuri na kadhalika. Lakini ni nini kipo nyuma ya yote hayo? Hebu tumpe nafasi…

**Tueleze kwanza jina lako na wewe mwenyewe…**

Jina langu ni Rose Camillius Nyandindi au Madam Rose kama wengi wanavyopenda kuniita.
Mimi ni mwalimu wa shule za sekondari, yaani kidato cha kwanza hadi cha sita. Nimebobea zaidi katika masomo ya Lugha *(Kingereza na Kiswahili)*
Nina shahada na stashahada ya ualimu.
Nimekuwa katika taaluma hii takribani miaka 20 sasa.
Mimi pia ni mwalimu wa ushauri na nasihi.



**Wengi nilioongea nao katika safu hii matoleo ya nyuma walisema kuwa siri yao kubwa ni vitabu, yaani kusoma vitabu. Vipi kuhusu wewe?**
Ni kweli, katika vitu napenda sana hata mimi ni kusoma vitabu. Ninapenda kusoma vitabu tangu nikiwa sekondari, nimekuwa nikisoma vitabu vya lugha mbili yaani kiswahili na kingereza.

**Kwanini umekuwa unapenda kusoma vitabu?**
Zipo sababu nyingi, ila nitaeleza chache;
Kusoma kitabu kwangu ni starehe na faraja.
Kwani ninaposoma ninaburudisha nafsi yangu na hunipunguzia msongo wa mawazo, kwani akili yangu huzama kwenye kile ninachokisoma.
Pili, kupata maarifa mbalimballi juu ya maisha na kujifunza mengi sana pitia wahusika na visa mbalimbali.

Pia,vitabu huniongezea maarifa ya kitaalamu na kitaaluma, kwani kwa taaluma yangu lazima niwe na wigo mpana wa maarifa. Na mwisho, mimi pia ni mwandishi, napenda kuandika andika vitu mbalimbali, tangu nikiwa sekondari. Wanafunzi wenzangu walikuwa wanavutiwa sana na tamthiliya na riwaya nilizokuwa naandika. Pia huandika mashairi.

Shairi langu la kwanza niliandika nikiwa darasa la. Nne alipofariki babu yangu.
Ilikuwa ni ajabu sana kwa wazazi wangu.
Na nimeendelea kuandika hadi sasa, kwani kupitia kazi za waandishi wengine naongeza ujuzi wa kisanaa.
Hivyo,hizo ndio sababu chache zinazonifanya nipende kusoma vitabu.

**Na ni vitabu gani unavypendelea kusoma?**
Napendelea kusoma vitabu vya kitaaluma, riwaya pendwa na tamthiliya .

Kama nilivyokwisha kueleza hapo awali, sababu mojawapo ya mimi kupenda kusoma vitabu ni kwasababu ya taaluma yangu.
Taaluma ya ualimu inahitaji sana maarifa mapya kila siku.
Ukizingatia mimi ni mwalimu wa lugha, kupitia vitabu napata misamiati mipya, maarifa mapya au ya ziada na ujuzi pia kwani kusoma ni mojawapo ya stadi za lugha yoyote ile.

Hebu tujuze, ni mwandishi gani unayemhusudu?
Mwandishi nanyempenda, nikitaja mmja nitapendelea, wapo wengi kwani husoma vitabu vya waandishi mbalimbali kutokana na maarifa ninayoyataka. Hivyo nitataja wawili wa ndani na wawili wa nje ya nchi. Ndani ya nchi napenda kazi za Shaban Robert na riwaya za kijasusi za Kamanda Amata. Nje ya nchi ni Robert Kiyosaki na David Oyedepo.

Watanzania, maarifa yanapatikana katika vitabu, zipo hekima nyingi sana kwenye makaratasi, usipofunua kurasa utabaki kama mfu, Elimu haina Mwisho. Siyo lazima ukae darasani ili upate maarifa, tujenge utaratibu wa kujisomea.

# MSALITI - 03

Na. Richard Mwambe

**Kitabu cha MSALITI sasa kinapatikana madukani. Jikamatie nakala yako uburudike.**

**Bei ni 15,000 tu. Wasiliana nasi kwa Whatsapp 0766974865.**

***Maelezo ya Kapteni Kituli yalimfanya Jenerali Mathurin kubaki kimya kabisa. Hakuwa na jibu la karibu, sembuse lile la mbali?***

Endelea…

Hata neno la haraka la kusema nalo lilimtoroka kana kwamba mfungwa amewapiga chenga Askari Magereza kwenye vichaka vya shamba walilopangiwa kufanya kazi. Mathurin alijaribu kuyameng'enya maelezo hayo aliyoyasikia kwa mara nyingine ili kupata picha halisi na kubwa. Si kwamba lilikuwa jambo jipya kwake lakini sasa alikuwa anajenga hali ya kuamini hayo anayoyasikia kutoka kwa Kapteni Kituli. Alimjua vyema mpiganaji huyu aliyepambana kufa na kupona na waasi hao miaka na miaka katika milima na misitu ya Jimbo la Kivu na maeneo yanayozunguka. Na bado yupo huko huko misituni. Ukimwangalia ni wa kawaida sana, lakini ukifika kwao huko Bandundu amejijenga kupita maelezo. Pamoja na kuwapo kwake msituni lakini hali iliendelea kuwa mbaya. Kwa nini?

Ana siri kubwa huyu! Mathurin akawaza, huku akimkodolea macho kapteni Kituli kana kwamba anamwona kwa mara ya kwanza au kaona kinyango.

"Haya, nipatie ujumbe ulioniitia," Mathurin akasema huku akiinua bilauri iliyojaa pombe na kujimiminia kinywani. Kapteni Moise Kituli 'Mutu ya Msitu' kama walivyozoea kumwita alijiweka sawa kwenye kile kiti alichokalia. Akavuta mkoba wake uliokuwa chini sakafuni na kuufungua. Ndani yake akatoa bahasha moja na kumpatia. Mathurin aliipokea na kuigeuzageuza kuangalia pande zote mbili, kisha akataka kuitia mfukoni. Lakini kabla hajafanya hilo mkono wake ukashikwa na Kituli.

"Isome!" Kapteni Kituli akamwambia Jenerali Mathurin, ambaye hakufanya pingamizi lolote. Akatulia kwa jozi la sekunde na kisha akachana pembeni mwa bahasha hiyo ili kuifungua. Ilikuwa na maneno kumi na mbili tu.

*'Baada ya kikao Kinshasa, tuonane Kampala, Jinja Hotel keshokutwa saa 11:00 Jioni,'*

Alipomaliza kuisoma, akaikunja na kuitia mfukoni na kuzungumza, "Sasa hii ndiyo mpaka umeniita huku?" Mathurin akauliza.

"Afande, unaona ndogo hiyo?" Kituli akauliza na kuendelea … "Hakikisha unafika katika kikao hicho, maana ni muhimu kwako… pia kitabadili maisha yako kamanda!" kauli hii ya Kapteni Kituli ilimfanya Mathurin kupata mshangao kidogo. Hata hivyo hakuthubutu kuuliza. Aliliweka moyoni. Baada ya mazungumzo ya dakika kama ishirini hivi wakaagana. Kituli alibaki palepale alipokuwa na Mathurin alielekea katika Hoteli nyingine huku kichwani mwake akifikiri juu ya ule ujumbe ambao haukuwa hata na jina la mwandishi. Kampala! Akawaza kwa mara nyingine. Kichwani mwake alijua wazi kuwa mwito huo si wa kawaida, kuna jambo, ukizingatia na lile aliloambiwa na Kituli.

❦

Katika ukumbi wa Makao Makuu ya Jeshi la DRC, kikao cha watu 6 kilikaliwa kikiongozwa na Makamu wa Rais wa nchi hiyo Mheshimiwa Kilian Mbote Mbote. Wengine watano waliobakia walikuwa ni makamanda kutoka kamandi mbalimbali ambazo zilikuwa

# MSALITI - 03



kwenye operesheni maalum. Wote watano walivalia sare za kijeshi. Kikao kile kilikuwa ni kwa ajili ya kutathmini hali ya usalama ya nchi ya DRC hususan huko Kivu ambako mapambano na waasi wa CRA yalipamba moto. Huko ndiko Jenerali Mathurin alikuwa akiongoza operesheni hiyo. Ni siku chache alikuwa hapa kuleta taarifa ya maendeleo ya usalama na sasa amefika tena kwa kikao. Ilikuwa ni kama usumbufu kwake. Lakini kwa wenzake walijua wanachokifanya.

"Katika mkutano wetu uliofanyika Addis Ababa, AU imekubaliana na UN kuwa kwa hali inayoendelea huko Mashariki mwa nchi yetu, inabidi kuongeza nguvu kutoka katika Jeshi la MONUSCO," Makamu wa Rais akaeleza.

"Kwamba wameona kuwa sisi tumeshindwa?" Jenerali Mathurin akauliza.

"Lazima ninyi kama makamanda wa juu wa jeshi mjue kwamba mapigano ya ukanda wote ule wa Mashariki ni mapigano ya kimkakati. Kinachoonwa si kilichokusudiwa. Na hii siri lazima muitunze kwa vifua vyenu, atakayesaliti hatokuwa hai hata kidogo," yule makamu aliongea na hata sura yake ilikuwa imebadilika.

"Sasa kama ni hivyo MONUSCO ikifika hali itakuwaje?" Kamanda mwingine akauliza.

"MONUSCO inakuja kulinda amani, ninyi nyote mnajua sheria za ulindaji amani zilivyo. Hawatakuwa na madhara sana kwa upande wetu…" akajibu.

"Ina maana jeshi letu tunaliondoa?" Mathurin akahoji kwa kimuhemuhe.

"Halitaondoka, kwa sababu kuna maeneo ambapo jeshi letu litacheza ngoma kubwa kuliko hilo la MONUSCO," makamu akaeleza.

"Nchi gani zitaunda MONUSCO?" mwingine akauliza.

"Kama mnavyojua kuwa ni nchi nyingi sana ambazo zinaunda MONUSCO lakini kwa kikosi kitakachofika hapa zitakuwepo Benin, Ivory Coast, Ghana, Afrika Kusini na Tanzania," akajibu.

"Mmmh!" mmoja wa wanakikao akaguna. Mguno ule ulimfikia makamu wa rais.

"Vipi?" akauliza.

"Na Tanzania wapo? Hawa watu mimi siwapendi kabisa…" akasema yule mwanakikao.

"Najua, lakini tutaona jinsi ya ku-deal nao, mipango yetu lazima iende kama tulivyopanga, haiwezi kubadilika!" yule Makamu wa Rais akawaeleza. Baada ya saa moja ya kikao kile kumalizika na mikakati stahiki kupangwa, hatimaye kilifika tamati. Kila mmoja akatakiwa kuondoka na kuendelea na majukumu yake.

*Itendelea toleo lijalo...*




Kitabu MSALITI kipo madukani, jikamatie nakala yako kwa Tsh 15,000 tu.

Tembelea duka la Kona ya Riwaya Kinondoni au piga

**simu namba 0655428085**
**Whatsapp 0766974865**

Jikamatie nakala yako sasa

# HADITHI: Najutia Kuwa na Wewe—02

MTUNZI: ASHA SIRAJ
Whatsapp 0789044345



*UTANGULIZI*

**Mapenzi sio kitu cha kuwekea maanani sana kwasababu ipo siku yanaweza kukuletea shida huko mbeleni, kuna baadhi ya changamoto nyingi hutokea. Hivyo ukisema kila jambo uliwekee maanani basi mapenzi yako yatabaki kuwa na majuto siku zote. Kutana na binti SHAZMA aliyepitia mateso mengi kwenye mapenzi yake na kujikuta akijutia kwanini amkabizi moyo wake mwanaume asiye na fadhira**

Siku zilizidi kusonga mbele nimiezi sita sasa toka nianze kuishi na shangazi, nakumbuka tulikuwa tukila shule huko huko, kama unavyojua chakula cha shule kilivyo wanafunzi niwengi sana ila chakula nikichache.

Kiufupi sikuwa nashiba hivyo ilinilazimu nikirudi nyumbani basi walau niweza kupata chakula kingine, ila shangazi yangu hakuwa tayari kunipatia chakula

Alimthamini sana binti yake Munira kuliko mimi, hivyo nilirudi nyumbani nakukuta vyombo vikinisubilia kwenye karo, sikuwa napata hata mda wakupitia masomo yangu kutokana na kazi nyingi kuninyemelea sana.

Kwa umri nilikuwa nao sikupaswa kufanya kazi nzito kama hizo, nilikuwa mtu wa kulia kila siku aswa nilipowakumbuka wazazi wangu, hicho kitu kilinipa wakati mgumu sana.

Nilikuwa nimezoea maisha ya madeko sana, ila ndo kama hivyo maisha hubadilika hata kwangu yalibadilika vile vitu ambayo vilikuwa vinanipa furaha viliondoka kwenye maishani yangu nilibaki mpweke tu.

Munira alikuwa mtu wakunidhalilisha shule kwa marafiki zake kuwa mimi nimasikini mimi sana hata kwao pia nipo kama mfanya kazi wa ndani,

Marafiki zake walikuwa watu wakunicheka nakunizodoa kuwa sifai kusomea shule ya pesa kama hiyo nawala sina hadhi hiyo

Kiufupi maisha yangu yalikuwa yagiza mpaka nihisi bora hata nami ningelibaki kwenye nyumba yetu nikafa kama wazazi wangu kwaasababu sikuona umuhimu wakuendelea kuisi duniani

Siku zilizidi kusonga mbele nimiaka mitatu imepita sasa mpaka pale nipofika darasa la saba nilianza kujitambua ila shangazi hakuacha kunisimanga, ila mume wake alikuwa mtu wanifariji kila wakati

Nilitamani walau mume wake ageuke kuwa shangazi yangu,ila haikuwezekana, nashukuru sana shule nilikuwa na akili sana kuliko huyo mwenzangu

Aliyekuwa akinisimanga kila siku kuwa sina hadhi ya kusomea shule za pesa kama hizo, nashangaza yeye aliyekuwa nahadhi alikuwa akishika nafasi za mwisho Yani nafasi zisizoeleweka

Maisha yangu yalizidi kuwa maisha ya chanagamoto ila ilifika wakati nikaanza kuzoea maisha hayo, japo haikuwa rahisi ila mimi kwakuwa niiamza kuyapitia nikiwa darasa la nne hivyo ilifika wakati nikayazoea rasmi

Mtu ambaye namuombea mpaka sasa nimume wa shangazi yangu ndiye mtu akiyenipambania sana, japo shangazi hakuwa anapenda vile alinavyinisaidia

Nakumbuka tulifanya mtihani wa moco wilaya nilipata ufaulu mzuri sana na kumzidi mwanzangu

Mumewe wa shangazi yangu baada ya kugundua nimepata ufaulu mzuri basi alinunulia vifaa vya shule pamoja na sale mpya bila kusahau na begi zuri.

Ila shangazi yangu kutokana na roho mbaya aliyokuwa nayo alininyanganya begi hilo nakumpatia binti yake Munira,

SHAZMA aliniita nakuniambia" huna hadhi ya kubeba begi zuri kama hili, kama unaona unashida na begi basi nenda makaburini kawambie wazazi wako wakununulie begi zuri kama hili, kama wanakupenda mbona walijua kukuacha

Itaendelea.... usikose kufuatilia kisa hiki nikisa kizuri sanaSehemu ya tatu

Ilipoishia
SHAZMA aliniita nakuniambia" huna hadhi ya kubeba begi zuri kama hili, kama unaona unashida na begi basi nenda makaburini kawambie wazazi wako wakununulie begi zuri kama hili, kama wanakupenda mbona walijua kukuacha.

Songa nayo...
Kusema ukweli maneno yashangazi yangu yalinikosesha amani sana, nakuamua kumuuliza?

Hivi shangazi nikitu gani nimekukosea mimi mpaka kuamua kunifanyia mambo yahivi? Kosa langu wazazi wangu kufariki au kosa langu nimimi kuwa hapa?

Oohh shabashi kumbe unajua kosa lako, alisema ngea shangazi nikabaki kumtazama, bora ulilivyolijua kosa lako kwanini usiwafuate wazazi wako huko walipo maana kwangu nisawa unanijazia choo tu nawla hauna kitu cha maana ambacho wewe unakifanya humu ndani

Nilipokuwa nimesimama nilihisi gazi ya gafla kwenye miguu maana sikutegemea kama shangazi angeweza kuongea maneno mazito kama hayo

Hata kama hajanizaa yeye ila hakupaswa kunimbia maneno makali na magumu kama hayo,

Unashangaa nini si ubebe kilicho chako uondoke hapa, nilimjibu shangazi hayo maneno hukupaswa kuyasema wewe bali hayo maneno alipaswa kuyasema mume wako ambaye hana undugu na mimi nawala sio wewe shangazi.


Kama ulikuwa hunipendi ilikuwaje ukanichukua na kunilea kama ulikuwa unaona mimi sifai kuwabhumu ndani basi ungeniacha kulekule kwasababu sina umuhimu mimi kuwa hapa.

Shangazi aligeuka nakutizama kwa macho makali sana, kama mbwa aliugua nakichaa vile hadi niliogopa, mimi ni ndugu yako tumezaliwa tumbi moja hivi akili zako zipo kweli kichwani mwako

Ukweli nilihisi kuzimia kwa maneno ya shangazi, hivi huyo Nishangazi yangu ninayemjua mimi au, kipindi nikiwa mdogo sana kabla ya wazazi wangu hawajafariki alikuwa ananipenda sana nilishangaa sana kumuona hivi sikutegemea kabisa.

SHAZMA hufai kabisa kuletewa vitu vizuri kama hivi, hivi vitu alifaa apewe mwanangu nawala sio wewe mchawi mkubwa wewe.

*Itaendelea toleo lijalo...*



# Ya Kale Ni Dhahabu– Alibaba na Wezi 40 (18)

"Kuna mtu anajaribu kukuua, bosi," Marjane alijibu. "Kuna siku niliona alama nyeupe ya chaki kwenye mlango wa mbele wa nyumba yetu. Nikajua huenda kuna mtu ameweka alama hiyo kwa siri na pia nikajua tu kwamba kuna kitu kibaya kinaendelea, hivyo nikaamua kuweka alama kama ile katika kila mlango wa mbele wa nyumba zote za mtaani hapa."

"Siku nyingine nikaona alama ndogo nyekundu kwenye fremu ya dirisha. Basi nikafanya vilevile katika nyumba za mtaani."

"Sasa jana," Marjane aliendelea kuelezea. "Muuza mafuta alikuja na punda wake ishirini na mitungi ishirini ya mafuta kama unavyojua bosi. Usiku wa jana ulipokuwa umelala, niliamua kuandaa chakula cha leo mchana kabisa, hivyo nilihitaji mafuta zaidi kwaajili ya taa ya chemni, hivyo nilienda kule uwani kwenye mitungi ili nichukue mafuta kidogo tu kutoka katika ile mitungi. Sasa nilipoenda kwenye mtungi wa kwanza ili nichukue mafuta. Nikaanza kufunua mfuniko wa mtungi, mara nikasikia sauti ikitoka ndani ya mtungi ikiuliza, "Vipi muda tayari tutoke kwaajili ya mapambano?"

Marjane alinyamaza kidogo akimuangalia Alibaba. Kisha akaendelea kuelezea. "basi sikuwa na cha kufanya. Ila nikaijibu ile sauti iliyouliza nikasema 'Bado – ila muda mfupi tu nitawajulisha!' nikaenda kwenye mtungi wa pili, hali ikawa ni ileile, na wa tatu pia—na wa nne na wa tano mpaka mitungi thelathini na tisa hali ilikuwa ni ileile na mimi nikajibu vilevile kwa sauti nzito kidogo inayofanana na ya muuza mafuta. Isipokuwa mtungi wa arobaini ndio uliokuwa na mafuta ndani. Nikajua tu kwamba kwa hali ile bosi wangu uko hatarini hivyo nikachemsha mafuta mengi sana yaliyotoka kwenye ule mtungi wa arobaini na nikayamimina katika kila mtungi. Nafikiri bosi sasa unaelewa stori nzima."

Alibaba alishtuka sana kusikia hivyo. Alisimama kwa muda kidogo kimya na kufikiri kwa haraka sana.

"Sina adui yoyote hapa mjini," Alijisemea moyoni. "Lakini kuna hazina niliziiba kutoka kwenye lile pango la ajabu msituni na wezi walimuua kaka yangu Kassim. Sasa nafikiri wanajaribu kutaka kuniua na mimi. Lakini hawatafanikiwa!"

Kisha akasema, "Umefanya vizuri sana Marjane. Umeokoa maisha yangu. Nafikiri huyu muuza mafuta ni kiongozi wa wale wezi waliomuua Kassim, nafikir wanataka kuniua na mimi kwasababu nilichukua dhahabu zao. Lakini yuko wapi sasa huyo muuza mafuta?"

"Sijui, bosi," Marjane alijibu. "Hata chumbani hayupo, nafikiri alikimbia usiku."

Ulipoungia usiku, wakati mkewe amelala, Alibaba alimuita kijana wake Khalid na wakachukua masepetu mawili na kuchimba shimo kubwa sana chini ya bustani yao. Katika shimo hilo, waliwazika wezi wote thelathini na tisa pamoja na mitungi yote arobaini. Lakini walizificha panga zao na mikuki ndani ya nyumba kwasababu walijua kwamba huenda kuna siku watazihitaji.

Asubuhi, Alibaba aliwaswaga punda wote ishirini sokoni na kuwauza wote.

"Nimewazika wezi wote thelathini na tisa na mitungi, na nimeficha silaha zao," Alibaba alimwambia Marjane. "Pia nimeuza punda wote ishirini. Lakini bado kuna tatizo moja. Kiongozi wa wezi bado yuko huru! Huenda akajaribu kuniuwa tena!"

Wakati ule, kiongozi wa wezi alikuwa amejificha msituni ndani ya lile pango. Akiwa ameshika tama kwa huzuni.

Baada ya kukimbia kutoka kwa Alibaba, alielekea moja kwa moja mpaka msituni. Alikuwa na hasira na aibu pia kwasababu mpango wake ulishindikana.

Bado kulikuwa na hazina nyingi sana katika pango. Lakini hili halikumfurahisha. Alikuwa mpweke sana. Kwasababu watu wake wote waliuliwa kule kwa Alibaba. Hakuwa na mtu wa kuongea nae – hakuna mtu wa kumuheshimu – wala hakuna mtu wa kumwambia maneno mazuri. Alibaki tu kufikiria kwamba, ni lazima amuue Alibaba!!!!!

*Itaendelea...*

- Baadhi ya Wadau Walalamika



# TUZO YA TAIFA YA MWALIMU NYERERE YA UANDISHI BUNIFU YAUNGURUMA MSIMU WA TATU



Tarehe 13 ya Mwezi wa Aprili mwaka 2025, tukio zito na kubwa la ugawaji tuzo zinazojulikana kama 'Tuzo ya Taifa ya Mwalimu Nyerere ya Uandishi Bunifu' lilifanyika kama ilivyo ada katika msimu wake wa tatu ndani ya ukumbi mkubwa na wa kisasa wa The Super Dome, Masaki, jijini Dar es salaam.

Tukio hilo kubwa la kitaifa lilihudhuriwa na mamia ya wadau wa fasihi na waandishi bunifu kutoka kila pembe ya nchi. Kila mmoja akiwa na shauku ya kutaka kujua ni nani na nani walipenya kwenye kinyang'anyiro hicho na kujinyakulia zawadi nono ambayo Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kupitia Taasisi ya Elimu TET ilikuwa imeandaa.

Kabla ya ugawaji wa tuzo hiyo kwa washindi, tukio lilitanguliwa na mjadala maalum uliofanyika kuanzia saa kumi jioni ulioongozwa na Mgeni mashuhuri Prof. Ibrahim Noor Shariff, Mhadhiri Mwandamizi na Mchoraji maarufu kutoka Chuo Kikuu cha Sultan Qaboos, Muscat, Oman na kuhudhuriwa na waandishi bunifu pamoja na wadau wa fasihi ya Kiswahili.

Katika hotuba yake ya ufunguzi mbele ya Waziri wa Ujenzi Mh. Aballah Uledi aliyemwakilisha mgeni rasmi, Mkurugenzi wa Taasisi ya Elimu Tanzania TET Dkt. Aneth Komba alieleza faida zilizopatikana tangu kuanzishwa kwa Tuzo hii kuwa ni pamoja kuongezeka maandiko bunifu katika maktaba zetu na kukuza uchapaji. Aidha alitanabahisha kuwa vitabu vilivyonyakua ushindi katika msimu wa kwanza yaani diwani ya Mtare wa Ngariba ya Bw. Amiri Abdalla na riwaya ya Gereza la Kifo ya Bw. Hamis Kibari vimekwishachapwa chini ya kampuni ya Mkuki na Nyota na kusambazwa mashuleni..

Mwenyekiti wa Tuzo hiyo, Prof. Penina Mlama naye alithibitisha kuwa, tuzo hiyo imekua kutoka tanzu mbili katika msimu wa kwanza na kufikia nne katika msimu wa tatu.

Jumla ya washindi kumi na mbili walijinyakulia zawadi ya pesa taslimu na cheti cha heshima, na watatu kati yao walitunukiwa na ngao ya ushindi kwa kuchukua nafasi za kwanza kwenye kila tanzu huku wengine ishirini na tano wakipatiwa cheti cha heshima.

Washindi wa msimu wa tatu wapo kama ifuatavyo:-
Mshindi wa kwanza mpaka wa tatu upande wa Riwaya ni (1)Maundu Moris Mwingizi 'Jeneza la Taifa', (2)Majaliwa Ibrahim Sued 'Kuokoka' na (3)Lucas Gervas Lubango 'Bweni la Wavulana'.

Upande wa tamthiliya, mshindi wa kwanza mpaka wa tatu ni (1)Tyatawelu Emmanuel Kingu 'Alama ya Kuzaliwa', (2)Saidi Yusufu Kileo 'Mwangaza' na (3)Ignas Dennis Mkindi 'Mwale wa matumaini'.

Upande wa ushairi, waliyoibuka kidedea ni (1)Hussein Kondo Abdalla 'Urithi wa Mjumu', (2) Adili Ally Mwinyiae 'Yunge' na (3) Ally Bakari Mchanyato 'Tuzo ya Usomaji'.

Upande wa hadithi za watoto, kadiri ya vigezo vilivyowekwa haikuwa rahisi kupatikana washindi kumi kama tanzu zingine, badala yake ni washindi saba tu walipatikana kwenye orodha fupi. Kati yao watatu waliochukua nafasi za juu ni (1)Tune Shaaban Salim 'Maziwa ya Kuku', Shifaa Feisal Amin Ibuni 'Maua na Mji wa Maweni' na wa (3) Paulina Barnabas Lugabulila 'Dirisha la Ajabu'.

Pamoja na yote hayo wadau wa fasihi waliohudhuria tukio hilo wamelalamikia mambo mawili, na kusema wazi kuwa yameshusha hadhi ya msimu huu wa tatu. Mambo hayo ni pamoja na kuzingatia ratiba na kupunguza mlolongo wa hotuba na pili ni kuendelea kuweka ratiba ya chakula kama misimu ya nyuma.

Jarida la Ngurumo ya Mwandishi tunatoa pongezi sana kwa washindi na kamati nzima iliyoandaa tuzo hii.

© *Mwandishi wetu*

# HISTORIA YA VITABU ULIMWENGUNI—02

Katika mwendeleo wetu wa Historia ya Vitabu Duniani, toleo lililopita tuliona historia fupi na kuanza kuchambua vitabu vya kale. Katika toleo lile tulipitia kitabu cha EPI OF GILGAMESH kama ifuatavyo:-

1. **Epic of Gilgamesh** (karibu 2100 KK) – Hiki ni moja ya maandiko ya kwanza kabisa katika historia, kilichoandikwa kwa maandishi ya msumari kwenye vibao vya udongo huko Mesopotamia (Iraki ya sasa).

Katika toleo hili tunaendelea na kitabu kingine KITABU CHA WAFU.

## 2. Kitabu cha Wafu (Book of the Dead)

Kitabu cha Wafu *(Book of the Dead)* ni mkusanyiko wa maandishi ya kidini ya Wamisri wa kale, yaliyokusudiwa kusaidia roho za wafu kupitia ulimwengu wa akhera na kufanikisha maisha ya milele. Jina hili linatokana na tafsiri ya Wazungu (hasa Wajerumani) waliogundua maandiko haya karne ya 19, lakini jina halikuwa la asili ya Wamisri.

**Maelezo Muhimu kuhusu Kitabu cha Wafu:**

**1. Asili yake:**
- Kilianza kuandikwa takribani mwaka 1550 KK hadi 50 KK.
- Ni mkusanyiko wa nyimbo, dua, maagizo na matamshi ya kichawi.
- Kiliandikwa kwa maandishi ya *hieroglyphics*, *hieratic* au *demotic*.
- Mara nyingi kiliandikwa kwenye *papyrus*, na kuwekwa ndani ya kaburi pamoja na marehemu.

**2. Kusudi lake:**
- Kumsaidia marehemu kuelewa kinachotokea baada ya kifo.
- Kumpa mwongozo wa kuvuka vizuizi vya dunia ya wafu.
- Kuandaa roho ya marehemu kwa ajili ya hukumu ya mwisho – ambako moyo wake unalinganishwa na manyoya ya *Ma'at* (mungu wa haki na utaratibu).
- Kuimarisha nafasi ya marehemu kufikia Bustani ya Aaru (paradiso ya Wamisri).

**3. Maudhui Muhimu Ndani Yake:**
- Tamko la kutokuwa na hatia *(Negative Confession)*: Marehemu anasema dhambi ambazo hakufanya ("Sikuiba," "Sikuua," "Sikumwambia mtu uongo," n.k.).
- Mazoea ya kichawi: Matamshi ya kuwatuliza majini, kuzuia mitego, na kupata ulinzi kutoka kwa miungu kama Osiris, Anubis, na Ra.
- Maono ya Akhera: Maelezo ya maisha ya baada ya kifo, hukumu, na safari ya roho.

**4. Miungu Muhimu:**
- Osiris – mungu wa wafu na ufufuo.
- Anubis – mungu wa uimbaji wa wafu na mlinzi wa makaburi.
- Thoth – mungu wa hekima, mwandishi wa hukumu.
- Ma'at – mungu wa ukweli na haki.

**Mifano ya Vifungu maarufu:**
Tamko la Haki (kutokuwa na hatia):
"Sikutenda dhambi dhidi ya mtu yeyote. Sikuiba. Sikufanya uzinzi. Sikusema uongo..."

**Dua ya kuamsha roho:**
"Ee roho wangu, usinishuhudie kwa uovu mbele ya mahakama ya miungu..."

Unapovutiwa na Kitabu cha Wafu, unaweza pia kulinganisha na maandiko mengine ya kale kama vile:
- The Tibetan Book of the Dead (Bardo Thodol)
- Divine Comedy ya Dante (karne ya kati)
- The Epic of Gilgamesh (kwa maudhui ya maisha na kifo)

Katika toleo lijalo tutaendelea na makala hii ya historia ya vitabu ulimwenguni.

Muwe na sikukuu njema!

***Itaendelea...***

# KITABU NILICHOSOMA

## ISHI NDOTO YAKO (marudio)

**Jina la kitabu:** Ishi Ndoto Yako
**Mwandishi:** Joel Arthur Nanauk
**Msomaji:** David Rusato Ernest
**Mkoa wa Msomaji:** Kagera.

Kwenye kitabu hiki nimejifunza mbinu mbalimbali, ninazoweza kuzitumia ili niweze kukamilisha na kuiishi ndoto yangu, kama inavyoelezewa.

**1. Kuweka malengo makubwa ili uweze kuiishi ndoto yako.**
Yakupasa kujua unahitaji nini maishani mwako. Ukishajua weka vipaumbele, kwa kuonesha jambo la kwanza hadi la mwisho na kuviwekea mikakati sahihi ukilenga kufanya mambo makubwa hata ukishindwa utapata japo kidogo. Les Brown alisema "Lenga mwezi hata ukikosa, angalau utapata nyota"

**2. Kutambua jambo unalolipenda na kulifanya vizuri.**
Ndan yako kuna jambo unalolipenda na ukilifanya unalifanya kwa ustadi mkubwa bila hata kusimamiwa. Ukiligundua utapata matokeo makubwa kwa kutumia nguvu kidogo na utaweza kuiishi ndoto yako. Mfano Colonel Sanders alifanya mambo mengi bila mafanikio, alikata tamaa hadi kutaka kujiua. Lakin alipogundua kuwa kupika ndio kitu anakiweza zaidi,alifanya na kufanikiwa kuwa bilionea mkubwa dunian.

**3. Kuweka bajeti.**
Bajeti inakuongoza kujua mapato na matumizi yako, mfano Cyril Northcote Parkinson alisema "Matumizi huongezeka kulingana na kipato ili kumaliza ongezeko la kipato kipya". Hivyo bajeti itakusaidia kujua matumizi muhimu na ya lazima na sio pesa iliyopatikana.

**4. Kuwa na mtizamo chanya.**
Zitazame changamoto unazopitia kama funzo linalokuandaa kutimiza ndoto yako. Ukiwa na mtizamo chanya utaweza kubadili changamoto kuwa fursa kwako. Mfano kanuni ya mabadiliko inasema "Hali yoyote unayoiona nje yako ni matokeo ya vile ambavyo uko ndani yako" Nick hakuwa na mikono wala miguu lakini alijiona kuwa anaweza kubadili kesho yake, alijifunza kutumia kompyuta na kuogelea, na aliweza kutembea duniani akiwatia moyo watu waliokuwa na changamoto.

**5. Kujifunza kwa walio tangulia.**
Ili uishi ndoto yako huna budi kupata maarifa mapya na ujuzi kutoka kwa watu waliofanikiwa. Hii itakusaidia kuipata dira sahihi na kufanya vizuri zaidi. Mfano Lionel Messi alikuwa anabaki na Ronalidinho kwenye uwanja wa mazoez akiwa anamfundisha kipiga "free kick" hatimaye Messi alikuwa fundi wa "free kick" ulimwenguni.

**6. Kutokughailisha mambo na kuchukua hatua.**
Jambo lililo ndani ya uwezo wako usilisubirishe, chukua hatua lifanye bila kungoja maana ili upate kitu ambacho hujawahi kupata lazima ubadilike ufanye kitu ambacho hukuwahi kufanya. Mfano Mark Twain alisema "Miaka 20 kuanzia leo utajutia zaid mambo ambayo hukufanya, zaidi ya yale uliyo fanya. Hivyo ishinde tabia ya kughailisha mambo ili uiishi ndoto yako.

**7. Ondoa hofu ya kushindwa na usikate tamaa.**
Haijalishi umeshindwa mara ngapi, ifuate sauti ya ushindi iliyoko ndani mwako. Jarib kufanya inaweza kuwa ni wakati wako, acha kulalamika. Ili ufanikiwe lazima hamu ya kufanikiwa iwe kubwa kuliko hofu. Mfano Martin Luther King alisema "Kama huwezi kuruka basi kimbia, kama huwezi kukimbia basi tembea,kama huwezi kutembea basi tambaa" hivyo yakupasa kuanza na ulicho nacho usisubiri kikubwa.

**8. Kuwa mvumilivu.**
Ili uishi ndoto yako huna budi kuvumilia maumivu, kukataliwa,na kubezwa lakini usivunjike moyo. Ili uishi ndoto yako changamoto ni daraja la kupitia. Mfano Nelson Mandela alivumilia mateso na kufungwa jela miaka 27, lakin baada ya kutoka jela, alizid kuipambania ndoto yake na hatimaye ilitimia alileta ukombozi Afrika ya kusini.

**9. Kutambua aina ya watu wanao kuzunguka.**
Ukishatambua watu wanao kuzunguka itakusaidia kuchagua watu sahihi wanaoweza kukusaidia kutimiza ndoto yako, na kuwaweka kando watu wenye mitizamo hasi na mawazo ya kushindwa, pia hii itakusaidia kujua aina ya boss uliyenae na kutafuta njia sahihi ya kufanya nae kazi bila kuaribu ndoto yako.

**10. Kujiamin na kuwa jasiri.**
Tambua kuwa wewe ni wa thaman na unaweza kutimiza ndoto yako, usikubali kukatishwa tamaa na watu, fanya kazi kwa bidii na utatimiza ndoto yako. Mfano kanuni ya Lucus Control inasema "kadri unavyojiona kuwa jambo liko juu ya uwezo wako na huwezi kulitatua, ndivyo ambavyo utazid kujiona huna thaman na utaendelea kukata tamaa". JIKUBALI



Mwandishi Fadhy Mtanga akichangia hoja katika mkutano wa awali kabla ya tukio la kugawa Tuzo.



Mabingwa wa Riwaya wa Tuzo ya Taifa ya Mwalimu nyerere ya uandishi Bunifu. Kutoka kulia ni Hamisi Kibari (Msimu wa kwanza), Laura Pettie (Msimu wa pili) na Mundu Mwingizi (Msimu wa Tatu) Wote hawa ni wana-UWARIDI




**Prof. Ibrahim Noor Shariff (katikati)**



**Mshindi wa kwanza Hadithi za watoto, Bi. Tune Shaaban (aliyeshika Tuzo)**




Furaha ya kumpongeza Mshindi wa kwanza wa riwaya msimu wa tatu Maundu Moris Mwingizi (aliyeshika tuzo)

TANGAZA na NGURUMO YA MWANDISHI kwa bei nafuu na ya kirafiki.
Matangazo madogo ni Tsh 5000@ na Tangazo la kurasa nzima ni Tsh 10000@.
Wasiliana nasi kwa simu *(call & Whatsapp)* 0766974865 na Email: jamvilasimulizi@gmail.com

UTEKAJI WA WATOTO (April '24)

Ynishangaza,
Ni katika giza,
Nani aloagiza,
Watoto wetu kutekwa?

Najiuliza,
Hofu yanihanikiza,
Uchungu kwangu najuza,
Hili limenikaa moyoni.

Eti nini?
Wayosema watungani,
Kwani hupo uzazini?
Huoni ya mtaani.

Unaropoka tu,
Unakosa wako utu,
Moyowo pomoni kutu,
Sura tu inakuhukumu.

Wasimama mbele yetu,
Wapaza sauti butu,
Eti wala hakuna kitu,
Ni uzushi tu watu.

Weweee!
Tumia yako hekima,
Fikiria kwa wako mtima,
Usiwe kipaza cha njama
Bali kipaza cha umma

Kama mmeshindwa basi tutafanya wenyewe!

@ Shujaa Maneno
Bagamoyo Pwani.

TAIFA LAENDA WAPI?

Vilio vyasikika
Wengine wanung'unika
Wengine walalamika
Wengine wameridhika
Eti' utu uko wapi?

Fulani kapotea
Hatujui lilotokea
Twabaki kukodolea
Masikio kuchokolea
Eti' utu uko wapi?

Hebu twambieni, sisi umma wa Tanzania
Kwani mwatufichani, ndugu zetu twalilia
Leo katekwa nani, kesho nani kapotea
Twataka mtueleze, Taifa laenda wapi?

Mama yetu Tanzania, watu wanakuchafua
Rais wetu Samia, kinywa chako fungua
Watoto wako twalia, nani wa kututetea
Twataka mtueleze, Taifa laenda wapi

Nyumani tulisifiwa
Sifa nyingi tukaimbiwa
Tanzania tulikuwa
Mfano wenye kuigwa
Kisiwa chenye amani, ki wapi duniani?

Mikono ilojaa damu
Yatsalimu pasi hamu
Ukiwaona wanadamu
Lakini mioyo yawahukumu
Ile nchi iko wapi?

©Shujaa Maneno
Bagamoyo Pwani

Unaweza kuchangia chochote ili kuwezesha jarida hili kuwa bora na kuwafikia wengi zaidi. Kama upo tayari, changia kiasi chochote kupitia MPESA LIPA NAMBA 5559006 JAMVI LA SIMULIZI. Na Mungu atakujazi.













Jenga tabia ya kusoma vitabu kila upatapo muda. Vitabu vyetu vinapatikana

Duka la Kona ya Riwaya Kinondoni - Simu namba 0655428085
Posta Mpya Dar es salaam karibu kabisa na mzunguko wa Sanamu ya Askari kwa Joji - Simu 0713454152
Morogoro Morena hotel, Stendi ya Dalala Smaki Samaki na Bima kwa Markus Mpangala - Simu 0719226293
Au wasiliana nasi Jamvi la Simulizi kwa Whatsapp Namba 0766974865

# KUTOKA MAKTABA:MAISHA NI MAPAMBANO—9

**Hiki ni kitabu kilichoandikwa miaka mingi sana nyuma. Kiliandikwa ili kiweze kusomwa na watu mbalimbali na kuwekwa kwenye maktaba za vijijini. Tunakitoa kutoka kwenye maktaba yetu ili kukupa uhondo, Ngurumo ya Mwandishi ni kisima cha fasihi chenye hazina iliyotukuka.**

## TAMAA YA UTAJIRI WA HARAKA HARAKA—9

### SURA YA 3
### Kisomo na maendeleo kijijini

Pia kusukumwa kwa ajili ya faida yake aliona ni kitendo haramu na sio utu. Aliwalaani wote wenye vitendo hivyo.

Bidii za Mpepo na mkewe zilianza kuonesha matunda baada ya muda mfupi. Badala ya kuwa na shamba lenye ekari mbili, waliliongeza hadi kufikia ekari tano. Kulikuwa na mazao ya aina nyingi; minazi, mahindi, maharage, kunde, mihogo, michungwa, mpunga na mazao mengine. Mazao yote hayo waliyagawa katika sehemu mbalimbali. Mengine ekari moja, hasa ya chakula; na mazao mengine kwenye nusu eka au robo tatu ya eka hasa mboga. Pamoja na shughuli zake za shamba pia alishiriki kikamilifu katika maendeleo ya kijiji hasa kisomo. Shamba lake lilistawi sana kwa vile alikuwa akifuata sana maagizo ya wataalamu wa kilimo. Kuna wakati mmoja aligombana na jirani yake kuwa yeye ni mchawi. Alimshutumu kwamba alikuwa akiyavuta mazao yake na kuyapeleka kwake kwa njia ya uchawi. Ukweli ni kwamba utaalam wa kilimo au kilimo cha kisasa ndiyo ulikuwa uchawi wenyewe. Jirani alikuwa bado mjinga. Kuthibitisha ujinga wajirani yake, wakati mmoja alilalamika sana juu ya dawa ambayo alipewa na mganga mmoja wa kienyeji. Aliambiwa aweke mayai mabovu kumi kuzungushia shamba kama kinga kwa wadudu waharibifu, wezi, wanyama na kukomesha balaa nyingine zote. Kinyume cha mategemeo yake wakati wa mavuno aliambulia gunia moja tu maana karibu shamba lote lilishambuliwa na wadudu. Kwa ujinga wake aliendelea kumlaumu Mpepo kwamba yeye ndiye kisirani na ndiye aliyewatuma wadudu wale mazao yake.

Mpepo alijulikana sana pale Tetere kwa hadithi zake za kutisha kuhusu maisha yake ya siku za nyuma. Alikuwa akiwasisitizia majirani zake kwamba katika kazi zote halali kilimo ilikuwa ni 'Uti wa mgongo'. Mbali ya kwamba maneno hayo yamesemwa na watu wengi, baadhi yao wakiwa viongozi, Mpepo alisema, amekiri na kuthibitisha katika muda mfupi tu tangu aanze maisha mapya. Aliongeza kwamba binadamu au kiumbe chochote bila kuwa na uti wa mgongo hakuna uhai.

Siku kadhaa zilipita, Mpepo alichaguliwa kuwa mjumbe katika halmashauri ya kijiji chao. Kijiji kilikuwa kimekamilika kwa huduma na vyombo vinavyohitajika; jumuia za chama, kamati za utendaji zote - yeye aliteuliwa kuwa mjumbe wa kamati ya shule pia. Hata hivyo alishiriki sana kwenye maenedeleo ya shamba la kijiji. Lengo lake hasa lilikuwa kupata maagizo zaidi ya wataalamu wa kilimo ili aweze kuyatumia katika shamba lake.

Kwa bidii za akina Mpepo na wanakijiji wote, kijiji kilipata maendeleo mazuri sana. Kilipata mashine ya kusaga ambayo iliwarahishia akina mama wa kijijini na vijiji vya jirani kazi ya kwenda mbali kusaga unga au kusaga nafaka kwa mawe. Ilijengwa zahanati nzuri ambayo iliendeshwa na vijana wa pale kijijini waliopatiwa mafunzo ya uganga. Siyo hivyo tu bali kijiji kilipata mashine ya kusukuma maji na ya kupasua mbao iliendeshwa na vijana waliopatiwa mafunzo kwenye chuo cha maendeleo ya wananchi cha jirani. Vilevile walianzisha mradi wa ng'ombe wa maziwa na mifugo mingine.

Shamba la kijiji lilikuwa na mchanganyiko wa mazao. Mazao ambayo yalitengwa katika maeneo mbalimbali kufuatana na aina ya mazao. Hawakuwa na shida ya kuuza mazao yao kwa sababu palikuwa na chama chao cha ushirika ambacho kilinunua mazo ya shamba la kijiji na hatimaye kuuza kwa vyama vingine. *Itaendelea..*

# TAMASHA LA TAFF MSIMU WA TATU

## "Rudisha Kitabu Nyumbani"

**Na Mwandishi wetu**

'Hayawi hayawi, yamekuwa' huu ni msemo wa wanafalsafa wetu wa Kiswahili ambao sisi hupenda kuwaita 'Wahenga' ukimaanisha kuwa lile tulilolisubiri kwa hamu sasa limetimia. Ni Tamasha la Mfuko wa Fasihi Tanzania mara hii linakuja kwa kishindo.

Jarida lako pendwa la Ngurumo ya Mwandishi ambalo daima limekuwa likiimulika fasihi ya Kiswahili kwa namna tofauti lilikutana na Afisa Habari wa Taasisi hiyo Ndugu Stallone Joyful na kufanya mahojiano mafupi juu ya tukio hili kama ifuatavyo:

*Swali: Bwana Stallone, Watanzania na wapenda fasihi kote duniani ambko jarida hili husomwa wana hamu ya kujua kuhusu hili. Hebu kwanza tupe historia ya TAFF na Tamasha la Fasihi kwa ujumla. Yaani wazo lilikujaje na ilikuwaje?*

Jibu: Mfuko wa Fasihi Tanzania au kwa kiingereza (Tanzania Fasihi Fund –TAFF) Ni taasisi iliyoanzishwa ili kuihuisha na kuendeleza fasihi kama zana muhimu ya maendeleo kifikra, kuondoa ujinga na kuleta maendeleo ya mtu binafsi, jamii na taifa kwa ujumla. TAFF itajenga uwezo wa watunzi wa kazi za kubuni za fasihi, kuinua vipaji, kuibua vipaji vipya katika eneo la fasihi, kundeleza vilivyopo na kuhakikisha fasihi inakuwa zana muhimu ya maendeleo ya jamii, taifa na nchi kwa ujumla.

Tamasha la Fasihi ni mojawapo kati ya mambo kadhaa yaliyopelekea kuanzishwa kwa Mfuko wa Fasihi Tanzania. Hili ni tukio la siku kadhaa ambalo huanza na shughuli mbalimbali na kuja kuhitimishwa siku ya mwisho ambapo huwa na mijadala ya kina yenye maslahi kwa watunzi, uzinduzi wa vitabu, kuzawadia waliofanya vizuri katika fasihi, kusherehekea mafanikio pamoja na kupaza sauti kwa jamii na wadau ili fasihi ipate nafasi inayostahili.

Wazo la kuwa na Tamasha la Taff lilikuja baada ya kugundua kwamba hakukuwa na ulingo wa kina wa wanafasihi kukutana na kujadili masuala yao. Hivyo tuliamua kuwa na Tamasha hili ili kufanya jukwaa la wanafasihi kwa malengo ya kukuza fasihi ya kiswahili Tanzania na Afrika kwa ujumla. Kuwakutanisha waandishi wachanga na wakubwa kujadili mada zenye mawazo ya kuendeleza ubora wa fasihi ya kiswahili. Hili ni Tamasha la Tatu, Tamasha la kwanza na la pili yalifanyika mwaka 2021 na 2022 katika wilaya ya Kisarawe mkoa wa Pwani katika viwanja vya Chanzige.

*Swali: waoh, hongereni sana. Sasa, je kuna mafanikio yoyote tangu muanze kufanya Tamasha la Fasihi ya Kiswahili?*

Mafanikio ni mengi kwa hakika na kwa kweli yanamwagika, tumeweza kuibua vipaji vya vya utunzi wa hadithi kwa wanafunzi 12 mpaka sasa. Sita kutoka shule za Msingi na Sita kutoka shule za Sekondari. Jumla ya vitabu viwili vyenye mkusanyiko wa hadithi za washindi kwa mwaka 2021 vimechapishwa na kusambazwa katika maeneo mbalimbali.

Tumeweza kujadili masuala mazito na kuwasilisha maazimio yetu kwa wadau na kwa sasa fasihi inaanza kupata heshima yake inayostahili. Tunao wanaharakati wa fasihi, vyombo vya habari vya fasihi, matukio ya kifasihi makubwa nchini ambapo tunaamini hizi ni juhudi za wanafasihi wote ikiwemo TAFF. Mashindano tuliyoendesha yamechangia katika eneo kubwa kutoa mawazo yanayosaidia jamii na wadau wake kufikia ustawi. Tumeweza kufika mashuleni na kuwapa nafasi wale ambao wanatamani kuandika na hawajui pa kuanzia. Pia kuikuza fasihi ya kiswahili kwa kuibua hoja na mijadala kwa mada tulizokuwa tukiziendesha katika matamasha yaliyofanyika mwaka 2021 na 2022.

Katika mashindano tuliyoendesha, sio tu washindi walipata tuzo pamoja na fedha taslimu, bali pia walipata nafasi ya kuonekana na kuonyesha vipaji vyao, ambapo wengine ni waandishi mpaka leo hii.

Aidha kuungwa mkono na taasisi kubwa kama BAKITA, BAKIZA, COSOTA, MFUKO WA UTAMADUNI na Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo nalo ni eneo jingine ambalo tunaona ni mafanikio makubwa. Jukumu kubwa tulilonalo sasa ni kuhakikisha Fasihi inakuwa ajira na wanafasihi wanalipa

kodi ili Serikali ianze kutupangia bajeti katika mipango yake ya maendeleo.

Pamoja na mafanikio haya, mwaka 2023/2024 tulipumzika hatukufanya Tamasha hili kama ilivyo ada yetu, badala yake tulitumia muda huo kukaa chini na kujifanyia tathmini na kuboresha miundombinu ya tamasha na kuwa karibu na washika dau zaidi. Ndiyo maana mwaka huu tunakuja tukiwa na nguvu mpya ili kufanya tamasha bora zaidi, ambalo kwa kila hali litarudisha kitabu nyumbani.

*Swali: Enhee, rudisha kitabu nyumbani… bwana Stallone, palipo na mfanikio hapakosi changamoto, vipi kuhusu changamoto mlizokutana nazo na namna mnavyozikabili?*

Jibu: Watu wanatuelewa taratibu sana, tunachokifanya katika matamasha haya ni moja ya nane ya mipango yetu, tunatamani kuwa na tamasha kubwa lenye kujumuisha karibu kila mtu, tupate washiriki kutoka Tanzania nzima, nchi za Afrika Mashariki na dunia kwa ujumla, watu waiimbe fasihi ya Kiswahili na kuzitumia fursa zinazoletwa na kiswahili kuwa lugha ya saba ulimwenguni, lakini tunashindwa na gharama, hivyo kupitia chombo hiki cha habari tunaalikwa wadau tunaoweza kuungana nao kufanya Tamasha la aina yake ili tuweze kuwafikia watu wengi zaidi.

*Swali: Lengo hasa ni lipi la kuwa na Tamasha la TAFF?*

Jibu: Tamasha la Fasihi ya Kiswahili ni jukwaa la kipekee linalofanyika mara moja kila mwaka. Ni jukwaa la wazi linalowaleta pamoja watunzi wa kazi za ubunifu za fasihi, waandishi wa vitabu, wachapishaji, wasomaji, wachambuzi, wahakiki, wanafunzi, walimu, wanaharakati na watafiti wa fasihi ili kutafakari maendeleo ya fasihi nchini, barani Afrika na duniani, pamoja na hilo ni kufahamiana na kubadilishana uzoefu, kuwasilisha na kuonyesha kazi za fasihi, kujadili fursa zilizopo katika ulingo wa fasihi, kupanga malengo ya kukuza sekta ya Fasihi na kusherehekea mafanikio

TAFF inaamini kupitia Tamasha hili na kwa kushirikiana na wadau mbalimbali tunaweza kuleta mapinduzi yakinifu katika Tasnia hii ya Fasihi Andishi na Fasihi Simulizi

Lengo kuu la Tamasha la Fasihi ya Kiswahili ni kukuza sauti ya pamoja ya wadau wa fasihi na kuhimiza ushiriki wao katika maendeleo ya kiuchumi, kiutamaduni na kijamii.

*Swali: Katika msimu huu wa tatu tutegemee Nini kipya katika Tamasha la TAFF*

Msimu wa tatu ni msimu wa Mapinduzi kwani ndio utakuwa msimu wa kwanza kufanyika nje ya Kisarawe na mkoa wa Pwani kwa ujumla. Msimu huu litafanyika tarehe 28 na 29' mwezi Mei mwaka 2025 katika kijiji cha Makumbusho Kijitonyama jijini Dar es Salaam. Pia ni msimu ambao tulisogeza mashindano kwa watunzi na waandishi ambao ni watu wazima na sio wanafunzi wa wa shuleni kama ilivyo misimu miwili ya nyuma.

Msimu huu tumetoa Elimu kuhusu bima kwa jamii kwa kutumia fasihi na hasa miswada iliyoshindanishwa. Mpango wa kutumia enao la bima unalenga kuisaidia Serikali kufikia lengo lake la kuhakikisha asilimia 80 ya watanzania wanafikiwa na Elimu ya Bima na asilimia 50 wanatumia huduma hiyo ifikapo 2030. Fauka ya hayo, pia tumetoa elimu kwa washindi 11 tuliowapata miongoni mwa zaidi ya watu 131 waliotuma miswada yao ili iingie katika shindano. Elimu iliyotolewa kwa washindi ni juu ya matumizi sahihi ya mitandao ya kijamii na kujitangaza, elimu kuhusu bima na pia waandishi wote hao watapata nafasi ya kutembelea baadhi ya vivutio kujifunza zaidi kuhusu utalii wa nchi na baadhi ya mila na desturi za makabila mbalimbali. Vile vile itakuwa ni mara ya kwanza kushirikiana na Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania – TIRA

Katika msimu huu nje ya tuzo za washindi, tutakuwa na tuzo heshima kwa wadau mbalimbali, mijadala yenye afya katika fasihi, utalii wa ndani na tutawakumbuka na kuwaenzi wanafasihi nguli waliotangulia mbele ya haki, pamoja na kuwatia moyo waliopo. Kwa kweli kwa mwaka huu ni zaidi ya Tamasha. Tunawasihi watu wajiandikishe kushiriki tamasha hilo kwa kutuma ujumbe mfupi katika namba hizi: +255 657 532 334 na 0717727504. Mwaka huu ni lazima vitabu virudi nyumbani.

Asante saana Bwana Stallone Joyfull kwa kutujuza haya. Haya wadau waa fasihi, namba hizo hapo juu, jiandikisheni kwa kutuma sms ili ijulikane nani na nani watakuwa pale. Asante na *all the best!*

# HAPPY NEW YEAR '05'—Twahir Yusuph

***Ilipoishia…***

***"Niko na wewe Vivi, na nimebakiza jambo moja kubwa la kufanya nikiwa kama mpenzi wako." "Naruhusiwa kulifahamu Babe." "Muda utafika, ondoa shaka" "Mmh, okay baby." wote wawili wakaendelea kuvitupia vinywaji vyao hivyo sehemu stahiki, kupitia vinywa vyao. Alikuwa Labi Kimati na mpenzi wake mrembo aitwae Vivi. Labi alikuwa rafiki mkubwa wa marehemu wawili, ambao zilitengwa roho zao kikatili na fedheha mno, ni Jax pamoja na Imraan.***

*Endelea…*

Tangu rafiki zake hao watangulie huko akhera mashimoni, amekuwa mtu wa kunywa na kustarehe, leo aliandaa tafrija fupi asiyoipa jina, ila lengo lilikuwa kupambana na mawazo, pamoja na upweke wa kuondokewa na rafiki zake hao wa karibu.

**SURA YA 5**
**URAFIKI WAO**

Kabla maisha yao hayajapitiwa na usafiri wa kifo uliowabeba vijana hao wawili, Jax na Imraan walilelewa pamoja, wazazi wao walikuwa na ujamaa mkubwa mno, hivyo nao waliishi kama ndugu hadi wanaudandia umri wa balekhe. Walipishana miezi saba tu kwenye uzaliwa wao, walianza masomo yao ya awali pamoja hadi kufikia chuo. Walifanana kimatendo na tabia, hadi kuwafanya watu wengi waliowazunguka kuwaita mapacha. Chuoni walipendwa zaidi hasa kwa uwezo wao mkubwa wa kimasomo na kuucheza mpira wa kikapu. Kupitia mchezo huo wakawa maarufu mno, hata kukitambulisha chuo chao kama mabingwa wakubwa waliohofiwa na kila timu.

Nje ya tabia zao za kawaida waliisujudia anasa *kitakatifu* bila najisi, hakuna fukwe ndani ya nchi yao ambayo hawakuigusa mchanga wake. Klabu za usiku ziliwazoea, pia hata nyuso zao zilikuwa zenyeji mbele ya miili ya wanawake wengi sirini. Kupitia anasa hizo, ndipo walipokutana na Labi Kimati, urafiki wao ulianzia ndani ya klabu ya usiku, Jax na Imraan walipoanzisha vurugu dhidi ya vijana wengine waliowazidi ubavu, yeye Labi akaingilia na kuwasaidia. Hiyo ndiyo siku uhusiano wao ulianza rasmi, kwa haraka wakaanza kulijenga tofali moja moja hadi kuiunda nyumba kubwa ya urafiki uliowavutia.

Wakawa wamoja, tena maswahiba wakubwa mno, hadi kupelekea Labi Kimati kuhamia chuo walichokuwa wanasoma wawili hao. Walishibana sio kidogo, kila mmoja alipajua anapoishi mwenziwe, urafiki wao ukapelekea familia zao kuwa na ukaribu, zikafahamiana. Kupitia masomo ya biashara waliyokuwa wakisoma, wote wakazibeba ndoto za kuja kuwa wamiliki wa kampuni kubwa ya utengenezaji wa nguo za kisasa nchini. Wakaishi ndani ya barabara ya ndoto zao. Walitegemeana na kupeana upendo mkubwa mno, na hivyo ndivyo ulivyokuwa urafiki wao.

* * *

Muda ulisogea, kiza kilishaingia tayari, tafrija ilitamatika, jumba likabaki na binadamu wawili tu, Vivi pamoja na mpenziwe Labi Kimati. Miili yao ilipambwa na mavazi mazuri yaliyowakaa vyema mno, Labi akivalia suti yenye rangi ya bluu, huku Vivi akipambwa na gauni jekundu lenye urembo wa kumeremeta. Unaweza sema ni maharusi kwa namna walivyovalia na kupendeza, walivutia mno kuwatazama.
"Babe, bado hujasema tunaenda wapi lakini." Vivi aliuliza akiwa mbele ya kioo, viganjani akishikilia mkufu aliokuwa akijipimisha shingoni mwake. Hakujibu Labi, alimsogelea na kusimama nyuma yake akimtomasa kiuno kimahaba, punde akaipandisha mikono yake juu na kuvigusa viganja vya Vivi pamoja na mkufu alioushikilia, taratibu akaanza kumvesha.
"Sijawahi kuiona picha ya Leyla iliyomzubaisha Majnun kwa uzuri wake hadi kumpenda sana, ila


nakiri wewe ni mrembo zaidi yake Vivi, umependeza hadi nakuonea gere." aliweka tuo akimgusa mabega Vivi wake. Tabasamu likachanua surani pa binti mrembo. Vivi, akaigeuza shingo yake pembeni na kuyainua macho yake mazuri akimtazama Labi, aliyeishusha mikono yake na kuishusha tena kwenye kiuno laini cha binti huyo. Huenda alihisi hafaidi, alijigeuza Vivi na kuvigusanisha vifua vyao, mboni zake zikiendelea kuitazama sura ya Labi kwa bashasha. Wakawa wanatazamana.

*"You look so handsome honey, I mosty love you, forevermore,"* aliongea akijilaza kifuani mwa Labi wakiwa wamesimama.
"Haya tuwahi nikakuchune ngozi Malkia wangu, tunachelewa." sauti yake iliambatana na tabasamu pana usoni mwa Labi, huku akivipitisha viganja vyake shingoni mwa msichana huyo mrembo. Kicheko hafifu cha furaha kikakichopoka kinywa cha Vivi huku akiinua shingo yake kifuani mwa Labi.
"Haya niache nimalizie basi, tuwahi huko nisipopajua laaziz wangu." Alimwacha, wawili hao walikuwa chumbani, Vivi akamalizia kujiandaa na safari ikaanza, ni mtoko ambao Labi pekee ndiye aliyeufahamu. Majira yalionesha kuwa ni saa mbili usiku, safari ya Labi na Vivi haikuchukua dakika nyingi sana barabarani wakiwa ndani ya usafiri wao. Dakika kadhaa mbele gari yao ilikuwa ikipiga honi mbele ya jumba kubwa na la kifahari kama walilotoka. Walifunguliwa, wakazama ndani ya jengo hilo geni kwenye mboni za Vivi, hakujua amepelekwa wapi. Labi akawa wa kwanza kuteremka, akazunguka upande wa pili na kumfungulia Vivi mlango wa gari hilo ghari mno.

Atake nini Vivi mbele ya mwanaume anayemtendea vitendo vinavyomfanya ajihisi mithili ya Malkia. Kabla hajateremka mrembo huyo, Labi akaunyoosha mkono wake akimuomba aushike, akaupokea Vivi. Macho yao yakitazamana, huku sura zao zikisheheni tabasamu la furaha lililozijaa nyuso zao hadi utamu, polepole Labi alianza kumteremsha mrembo huyo garini. Ilikuwa tendo juu tendo, hakumpumzisha kisura wake huyo Labi. Akamwekea mkono kwa mtindo wa 'ingiza twende Malkia wangu.' Vivi naye akaupenyeza mkono wake katikati ya mkono wa mfalme wake Labi, ulioweka egesho kiunoni. Polepole wakaanza kuzama ndani ya jumba hilo la kifahari. Muda mchache mbele, tayari nyayo zao zilikuwa zikiambaa juu ya ardhi la ndani ya jumba hilo, taa hazikuwa zikiwaka.
"Babe mbona kiza hivi?." kwa wasiwasi aliuliza Vivi.
"Hebu ngoja nitafute swichi mpenzi." aliongea akimwachia Vivi mkono.

Akiwa amesimama peke yake Vivi, ghafla sauti kama ya risasi au kupasuka kitu ikapaza kwa nguvu ndani ya jumba hilo. Ilimshtua na kufanya apige kelele akiliita jina la Labi kwa kurudia rudia. Kimya, Labi hasikiki. Aliita tena, bado utulivu ulitawala ndani humo. Wasiwasi ukaanza kumjaa, hofu ikamtanda binti wa watu hadi sio vizuri. Lile neno la kuchunwa ngozi likaanza bisha hodi kwenye woga wake. Ila pia hiyo sauti ni ya nini? Mbona Labi wake haongei tena! Akiwa hajatulia, tena katikati ya hofu na maswali ya alipo Labi wake na kilichomkuta, ghafla ile sauti aliyoisikia mara ya kwanza, sasa zikafuatana zikiwa nyingi na kupaza kwa kupokezana, aliogopa Vivi. Mara punde taa zikawaka, zilimshtua na kumfanya atoe sauti ya hofu. Ila muda huohuo alipigwa na butwaa, mbele ya mboni zake walisimama watu wengi aliowashangaa.

*Itaendelea ...*



# "SHEMEJI USIZIME TAA...! NAOGOPA UKIMWI...! - 05

Na. Charles Gululla

**"Are you serious" alinihojim nikamjibu ndivyo. Baada ya shughuli nzito ya kulijenga taifa, nilimrudisha Ray Mabibo. Tulipofika tu, Hilda aliyekuwa bado yuko salon alitoka na kuja kwenye gari.**
**"Afadhali umemrudisha, nilikuwa na wasiwasi…"**

*Endelea…*

"Afadhali umemrudisha, nilikuwa na wasiwasi , pengine umeamua kumchukua moja kwa moja,"
"Hapana shemeji, ruhusa hiyo sijapata,"
"Jitahidi, uoneshe jeuri, utapata"
"Basi poa, we subiri tu utaona" nilisema na Hilda akanipa mkono wake, nikasuhika. Ulikuwa nyororo na nikauminya kistaarabu, akacheka.
"Ok asante dear, mimi nishafika, tutaonana tena siku yoyote ya week - end, siku zingine nitakuwa niko chuoni. Ukinitaka nipigie simu" Ray alisema na kunipa namba yake ya simu, name nikampa yangu. Akanibusu, nami nikambusu.
"Bye dear" Ray alisema huku akishuka kichovu na Hilda alipomuona alivyochoka, aliguna.
"Bye shemeji," nilimuaga Hilda na kujifanya sijasikia mguno wake. Akanipa mkono, nikauminya, naye akaukuna! We! Hilda alikuwa na hatari huyu, dalili ya kukuna mkono wangu ilimaanisha jambo fulani. (mambo ya pwani) we muache tu. Tukaachana na nilipogeuza gari niliwaona Ray na Hilda wakiwa wameshikana mikono wakiingia salon.
"Tuta" la Hilda lilinichanganya tena, lakini nikapuuza na kuendelea na safari yangu. "Hilda ana mambo yule… kweli yule alwatan kama nduguye alivyosema, halafu mjanja mjanja sana… shemeji wa Darisalaama!" niliwaza huku nikimkumbuka Ray wangu.

Jioni moja baada ya kupita siku nne nilikwenda tena Mabibo Farasi. Nilikuwa nimeongea na Ray kwa simu akanifahamisha huenda angekuwapo Mabibo jioni ile. Kwa kutamani kwangu kumwona Ray "live" nilikwenda baada ya kumaliza kazi.


Kabla sijshuka kwenye ki-HIACE Hilda alitoka saloon na kuja nilipokuwa nimepaki gari kwa mwendo wa maringo. Tembea yake ilinichota akili na nikazidi kumpenda shemeji yangu. Alikuwa mpaka karibu yangu na kunirushi busu la mbali.

"Hallo D.K Mambo zako,"
"Poa, nawe shem habari za kazi,"
"Salama kabisa shemeji langu, tena afadhali umekuja, kuna kitu nataka kukwambia" Hilda alibwabwaja na nikagundua kuwa alikuwa amekunywa. Harufu ya pombe ilisikika waziwazi alipokuwa akiongea, pia macho yake yalidhihirisha wazi.
"Kabla ya yote, Ray yupo?"
"Hapa hayupo ila yupo mahali fulani anakungoja na ana mcheche huyo, sijui umempa nini"
"Acha utani, kweli Ray yupo!"
"Kama huamini twende nikupeleke." Hilda alisema huku akirembua macho na kuzidi kulegeza sauti. Nikamwambia azunguke, na aingie kwenye mlango wa mbele wa HIACE.
Yarabi toba! Hilda wakati anaingia, alinyanyua miguu yake na kubaki nusu uchi. Maungo yake yaliyonona aliyaanika nje na hakuhangaika kuyafunika, badala yake akanisogelea zaidi na kunikonyeza. Hatari kubwa.
"Kaa vizuri basi shemeji," nilimsihi.
Kwani we tabu yako nini, endesha gari," Hilda aliniamuru kilevilevi, nikalazimika kugeuza macho ili nisiendelee kuutesa moyo wangu.
"Ni sehemu gani tuendapo?" nilimuuliza.
"Wewe endesha gari nitakwambia tukikaribia, tuliza 'kitenesi' Ray yupo shemeji," alisema huku akinipigapiga mabegani. Nililazimika kuendesha gari macho nikiwa nimeyakaza mbele na kuepuka kumwangalia Hilda. Jinsi maungo yake alivyokuwa ameyaanika, uzalendo ungenishinda saa yoyote.
"Hebu simamisha gari hapo pembeni" Hilda aliniamuru baada ya mwendo usiozidi dakika ta-

no. Nikamtii na kusubiri maelekezo yake.
“Nilikwambia kuna kitu nataka kukuuliza, hebu niambie umempa nini Ray hadi anakuota na kukusifu kila siku,” Lilikuwa ni swali gumu ambalo sikutegemea kama Hilda angeniuliza. Nikaguna.
“Kwa vipi?” nilimuuliza kiuchokozi.
“Anakusifia sana kuwa wewe ni dereva mzuri, hebu na mie endesha niuone udereva wako,” Hilda alisema bila aibu na nikajua alishaongea mengi na binamu yake kunihusu. Balaa.
“Shemeji huko unakotaka, wewe siyo kwema, na tafadhali usilete utani” nilimwambia kwa ukali kiasi, nikijua kama nitamlegezea anaweza kunizulia balaa. Badala ya kunijibu alinyanyua mguu wake wa kushoto na kuupachika juu ya mguu wangu. Jinsi mwili wake ulivyokuwa wa moto. Na nilivyotazama ‘guu’ lake lilivyojaa, tena likiwa wazi mpaka karibu na maungio, nilimeza mate. Wazimu ulishanipanda na nikaamua nimuoneshe kazi, si alitaka kujua udereva wangu! Isitoshe, mimi huwa sipendi kuchezewa na watoto wa kike. Kwa kuwa palikuwa ni pembeni ya njia, na watu walikuwa wakipitapita, niliamua kuzima taa za ndani yagali ili ni….
Nikazima gari, na kuzima taa, nikahama kwenye kiti changu na kutaka kumbeba kumtupa kwenye viti vya nyuma.
“Shemeji usizime taa… naogopa!” alilalamika baada ya kuniona niko siriazi
“Sema tena nikusikie,” nilifoka kwa ukali.
“SHEMEJI USIZIME TAA… NAOGOPA UKIMWI” alizungumza kwa sauti legevu..
“Alaa kumbe” nilisema baada ya kusikia neno Ukimwi, ambalo liliyeyusha tamaa yangu yote na kuutoa urijali wangu. Nikapumua na kuwasha taa, nikamkazia macho Hilda. Alicheka na kunikonyeza, na kuendelea kukaa vilevile kihasara hasara. Nikasonya na kuwasha gari.
“Hilda unajua kuwa unaniingiza majaribuni ukaaji wako huo, utatuponza” nilimsihi.
“Ee si wewe unajiita dereva mzuri, endesha tuone” bado aliendelea kunikejeli. Nikazima taa ili tamaa isiendelee kunishika.
“Shemeji usizime taa… naogopa Ukimwi” alirudia tena kauli yake. ……. ***<u>Imalizie kwenye ukurasa wa 7</u>***



## Tangazo




**TAMASHA LA TAFF MSIMU WA TATU**

**Usikose kaatika Tamsha la TAFF msimu wa tatu. Tamasha litafanyika katika viwanja vya Kijiji cha makumbusho, Kijitonyama, Jijini Dar es salaam.**

**Siku ya Waandishi, Siku ya wasomaji, Siku ya wanafasihi**

**Ni tarehe 28/5/2025.**

**Tutumie SMS kupitia namba +255 657 532**




Baadhi ya vitabu vilivyoshinda katika Msimu wa kwanza wa Tamasha la TAFF

Baadhi ya vitabu vilivyoshinda katika Msimu wa Kwanza wa Tamasha la

**RUDISHA KITABU NYUMBANI!**

www.richardmwambe.com

JAMVI la SIMULIZI